SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



UKURASA 19

**RAIS** Ramaphosa apata UVIKO-19


Nipashe TESA
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Jumanne Desemba 14, 2021
Awamu sita kufungua mwaka na sekondari mpya za kata 214
HATARI WASICHANA VVU UMATI, ACTIONAID wanapotaja mbinu za kutumiwa kuwanusuru
ELIMU
NA ELIZABETH ZAYA, ALIYEKUWA MPWAPWA
HATARI MIMBA UTOTONI...
Ushuhuda binti, nduguze watelekezewa bibi, wasoma kupitia 'umachinga mkaa'
•Mdau elimu: Ninawanusuru kila wanapoelemewa

UKURASA 11

Nipashe
Jumanne Desemba 14, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580794
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

## MADAI KIRUSI KIPYA

# SERIKALI YAFUNGUKA

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan, akishuhudia tukio la utiaji saini makubaliano kati ya serikali na kampuni za uchimbaji madini za Black Rock Mining Limited, Strandline Resources Limited na Nyanzaga jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Rais Samia: Bado kuna utoroshwaji wa madini

UKURASA 2

## Rufani ya Sabaya kusikilizwa mfululizo

UKURASA 3

**MICHEZO** **BADRU APEWA MIKOBA YA LWANDAMINA AZAM FC** UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akihutubia katika Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu, yaliyofanyika ukumbi wa Sheikh Idrisa Abdulwakil Kikwajuni jijini Zanzibar. **PICHA: IKULU**

## MADAI KIRUSI KIPYA

# Serikali yafunguka


**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imefunguka kwa kuanika kila kitu kuhusiana na uwapo wa kirusi kipya cha Uviko-19 nchini.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema taarifa za kuwa kuna wimbi la nne la ugonjwa wa corona nchini siyo za kweli na kwamba wanaosambaza wanazitumia kama vita ya biashara na Tanzania.

Aidha, amewataka Watanzania kupuuza taarifa hizo ambazo zina lengo la kuharibu sura ya nchi duniani hasa kwenye biashara ya utalii, na kueneza taarifa njema kwa ajili ya kuvutia watalii na wageni wengi nchini. Majaliwa alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza kwenye mkutano wa 21 wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), ambapo alisema hadi sasa hakuna mgonjwa wa wimbi hilo na baadhi ya vyombo vya habari vya nje vinavyosambaza havina lengo jema kwa nchi.

"Sekta ya utalii ina mchango mkubwa sana, kwenye kipindi cha UVIKO-19 tuliyumba kidogo, lakini tukajiimarisha na kuanza kupata watalii wengi, na mataifa walituamini. Tukaanza kusikia watu wakisema oohhh...Tanzania watu 500 wamekufa, watu 200 wamekufa, ule ulikuwa ni mkakati wa kuidhorotesha nchi," alisema Majaliwa.



"Juzi mmesikia tena, watu wanaanza kusema Tanzania ni nchi hatarishi kwa ugonjwa mpya wa wimbi la nne, sisi hatuna mgonjwa wa wimbi la nne hata mmoja hospitalini. Yote hayo ni vita ya kibiashara, kwa hiyo sekta binafsi mtusaidie kusema hayo."

Desemba 5, mwaka huu, serikali kupitia kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Prof. Abel Makubi, alitoa ufafanuzi kuhusu kuwapo taarifa za Mtanzania aliyedaiwa kupatikana na aina mpya ya kirusi cha wimbi la nne la ugonjwa huo cha Omicron.

"Tumepokea taarifa iliyoripotiwa na vyombo vya habari vya India na kuenea kwenye mitandao ya kijamii kwamba nchi hiyo imegundua kuwapo kwa abiria mmoja aliyerudi nchini humo kutokea Tanzania mwenye anuwai mpya ya Omicron,"alisema na kuongeza:

"Hata hivyo, haijulikani kama abiria huyo alitokea moja kwa moja Tanzania au alipitia Tanzania kuelekea India, pia haijulikani alipita wapi kabla ya kufika India."

# Rais Samia: Bado kuna utoroshwaji wa madini

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema licha ya jitihada za vyombo vya dola kulinda rasilimali ya madini, bado kuna utoroshwaji.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika hafla ya utiaji saini wa mikataba minne kati ya Wizara ya Madini, Msajili wa Hazina, na kampuni za madini za Strandline Resources, Blackrock Mining, Nyanzaga Mining na Rita Diamond Ltd.

Aidha, aliiagiza Wizara ya Madini kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kuendelea kudhibiti utoroshwaji huo na kuhakikisha shughuli za madini zinakuwa na manufaa zaidi kwa Watanzania.

"Niwaombe wale waliotumwa kusimamia, badala ya kuwa wao ndiyo chanzo, wajirudi sasa walinde rasilimali yetu...kazi hii haitoweza kufanywa na vyombo vya usalama peke yao, tufanye wote kwa kuwa ndiyo tulioko huko, tunaona mienendo ya mauzo ya madini,"alisema.

Vilevile, alisema dira ya serikali ni kufikia mwaka 2025 sekta ya madini ichangie pato la taifa kwa asilimia 10 kutoka asilimia 6.7 ya sasa, na kwamba miradi iliyotiwa saini ikianza kutekelezwa inaweza kufikia malengo hayo.

Kwa mujibu wa Rais Samia, serikali iliamua kubadilisha vifungu vya sheria ya madini ili kuipa nguvu kumiliki rasilimali hizo kwa niaba ya wananchi, maslahi mapana ya taifa na wawekezaji.

"Kupitia miradi hii serikali itapata manufaa mbalimbali ikiwamo kodi, tozo, ajira, gawio, uuzaji huduma kwa kampuni ambao utafanywa na wafanyabiashara ndogo na kurudisha hisani kwa wananchi ambao miradi hii ipo," alisema.

### KUONGEZA THAMANI

Rais Samia alisema: "Rai yangu kwa wizara ni kuendelea kusimamia kikamilifu suala la uongezaji thamani wa madini yetu...nataka kusema hapa, suala la kuongeza thamani madini hapa nchini haliepukiki."

Kwa mujibu wa Rais Samia, faida ya kuongezea thamani nchini ni pamoja na fedha nyingi za kigeni kubaki nchini hivyo kuongeza ajira kwa Watanzania.

### DIWANI AMSHANGAZA

Vilevile, aliagiza ushirikishwaji wa jamii kwenye utekelezaji wa miradi inayoendelea kwenye maeneo yao ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima.

Alitolea mfano wa wakazi wa Kigamboni, Dar es Salaam kunakotekelezwa mradi wa kuchimba madini yatokanayo na mchanga wa Kampuni ya Strandline Resources kutokuwapo kwenye hafla hiyo kutokana na vurugu zilizojitokeza kabla zilizosababisha kutoelewana juu ya umuhimu wa mradi huo kwao.

"Wasipokuwa (wananchi) na uelewa ndipo kunapokuwa na ukorofi, nina taarifa kwamba ule mradi wa kuchimba mchanga huku Kigamboni na wakati wa kutambulisha wananchi wa Kigamboni hawapo hapa leo, na hawapo kwa sababu walishaanza vurugu wakiongozwa na diwani wao," alibainisha.

Aidha, Rais Samia alionyesha kutokufurahishwa na kitendo cha diwani huyo kuongoza wananchi wa eneo lake kufanya migomo zaidi ya mara moja.

"Na nina alama ya kuuliza na yule diwani, kwa sababu wakati tunafanya operesheni ya machinga, diwani peke yake aliyeleta vurugu ni huyo wa Kigamboni, aliyepinga machinga wasiondoke, lakini wakati wa mradi huu ni yeye ameongoza tena wananchi wa Kigamboni kuanza vurugu."

"Lakini ni kwa sababu hawajaelewa, kama tutawaelewesha wakielewa vizuri wataupokea mradi huu na wataulinda wakijua kwamba mapato yatokanayo na mradi huu watafaidika nayo,"alifafanua Rais.

### KUTUNZA MAZINGIRA

Rais Samia aliwataka wananchi kuzingatia sheria ya mazingira kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali hasa ya uchimbaji wa mchanga kwenye mito na baharini.

"Miradi hii hasa huu wa kuchimba mchanga baharini unashtua kidogo, sasa hivi kina cha bahari kimepanda, mchanga ule ndiyo unaozuia maji ya bahari kuingia kwa watu...uchimbaji wetu usipopangwa vizuri tunaweza kusababisha janga lingine la mazingira," alisema.

WAZIRI KABUDI

Awali, Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi, aliitaja miradi iliyosainiwa kuwa ni Strandline Resources ambao ni wa uendelezaji na uchimbaji wa madini ya mchanga wa bahari uliopo wilayani Kigamboni kupitia kampuni ya ubia ya Nyati Mineral Sands limited.

Nyingine ni Blackrock Mining wa madini ya Kinywe uliopo Mahenge Wilaya ya Ulanga, Morogoro kupitia kampuni ya ubia ya Faru Grasslight Cooperation na Petra Diamond Ltd ya uendeshaji wa mgodi wa almasi wa Mwadui uliopo wilayani Kishapu, mkoani Shinyanga kupitia kampuni ya ubia ya Wiliamson Diamond Limited

### WAZIRI WA MADINI

Awali, Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alimshukuru Rais Samia kwa kuipa msukumo sekta ya madini hadi kupelekea kusainiwa kwa mikataba hiyo yenye uwekezaji wa Dola bilioni 763 (Sh. trilioni 1.75).

Alisema chini ya uongozi wa Rais Samia, makusanyo katika sekta hiyo yamekua, jumla ya mauzo ya madini Sh. trilioni 4.75 zimekusanywa na kujipa uhakika wa kufikia lengo la makusanyo ya Sh. bilioni 600 kwa mwaka.

Pia ziara za rais za kuleta wawekezaji zimezaa matunda kwa kutoa leseni 2,277 za uchimbaji madini, kati yake 11,574 ni za wachimbaji wadogo huku 65 ni za uchimbaji mkubwa na wa kati huku leseni 876 za utafiti wa madini zimetolewa pia.

## HABARI KITAIFA



Naibu Katibu wa Mambo ya Nje wa Chama cha ACT- Wazalendo, Bonifasia Mapunda, akihutubia mkutano katika Kata ya Ngapa, Jimbo la Tunduru Kaskazini mkoani Ruvuma, mwishoni mwa wiki, wakati wa ziara ya Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu ya kuwashukuru wakazi wa jimbo hilo, walioshiriki uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Rufani ya Sabaya kusikilizwa mfululizo

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Arusha, Februari 14, mwakani, inatarajia kuanza kusikiliza mfululizo rufani ya hukumu katika kesi ya jinai iliyokuwa inamkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya na wenzake wawili.

Ole Sabaya kupitia kwa mawakili wake, walikata rufani mahakamani kupinga hukumu iliyotolewa Oktoba 15, mwaka huu, na Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, Odira Amworo.

Naibu Msajili wa Mahakama Kuu Kanda ya Arusha, Ruth Massam, akizungumza jana alisema kuwa rufani hiyo namba 129 ilikwenda kwa ajili ya kutajwa tu.

Naibu Msajili huyo, alisema kuwa Jaji atakayepangwa kusikiliza rufani hiyo dhidi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), atajulikana siku iliyopangwa ya kuanza kusikiliza kwa rufani hiyo.


"Ninaahirisha kesi hii ya rufani hadi Februari 14, mwakani na siku hiyo kesi itaanza kusikilizwa mfululizo na Jaji atajulikana siku ya kuanza kwa kusikiliza shauri hilo," alisema.

Katika rufani hiyo, mawakili wa utetezi waliwasilisha hoja 14 wakiieleza Mahakama Kuu kwa nini hawakuridhishwa na hukumu iliyotolewa awali na Hakimu Odira.

Mbali na Ole Sabaya washtakiwa wengine ni Silvester Nyegu na Daniel Mbura na walikuwa wakikabiliwa na mashtaka matatu ya unyang'anyi kwa kutumia silaha.

Awali akitoa hukumu hiyo, Hakimu Odira, alisema kutokana na ushahidi uliotolewa mahakamani, mahakama hiyo imewatia hatiani na kuwahukumu miaka 30 kwenda jela kwa kutenda makosa matatu.

Hata hivyo, alisema kosa la kwanza na la pili ni la unyang'anyi wa makundi pasipo kutumia silaha, na kosa hilo Sabaya na wenzake waliwatendea Numan Yasin na Ramadhani Rashi (mashahidi wa Jamhuri), katika duka la Mohame Saad liliko Mtaa wa Bondeni jijini Arusha.



Alisema kosa la tatu ni la unyang'anyi wa kutumia silaha ambayo washtakiwa hao, walimtendea Bakari Msangi, walimpiga, kumfunga pingu, kumtishia silaha na kumpora Sh. 390,000.

Alisema hakuna ubishi kwamba Sabaya akiwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mwenye mamlaka ya uteuzi alitenda makosa hayo kinyume na sheria.

Pia alisema kwa kuwa mikono yake imefungwa na sheria hawezi kutoa adhabu ya zaidi ya kifungo cha miaka 30 japokuwa wametiwa hatiani kwa makosa matatu na ambayo kila kosa kifungo chake ni miaka 30, hivyo watatumikia adhabu hiyo kwa pamoja.

Alisema kosa la kwanza, la pili na la tatu ni kifungo cha miaka 30 kwa kila kosa na wakati mwingine kifungo kinakwenda sambamba na adhabu ya viboko hivyo alikataa ombi la wakili wa Jamhuri kifungo kwenda sambamba na viboko.

Katika rufani hiyo, wakata rufani ni mawakili Mosses Mahuna, Edmund Ngemela, Faudhia Mustapher, Sylvester Kahunduka na Fridolini Bwemelo.

Kadhalika wajibu rufani kwa upande wa Jamhuri ni Wakili Mkuu wa Serikali, Tumaini Kweka, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Felix Kwetukia na Wakili Mwandamizi, Othmed Mtenga na Baraka Mgaya Wakili wa Serikali.

# Ahukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa mauaji

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Mwanza iliyoketi Geita imemhukumu mkazi wa Kijiji cha Kilombero Wilaya ya Geita, Pius Makeja (42), kunyongwa hadi kufa kwa kosa la kumuua Mary Shija kwa kumcharanga mapanga sehemu mbalimbali za mwili.

Hukumu hiyo ilitolewa na Jaji Mwanabaraka Mnyukwa baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo pasipoacha shaka.

Jaji Mnyukwa alisema mahakama hiyo inatoa adhabu hiyo dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na kwa watu wengine wenye tabia za kikatili.

Alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, James Pallangyo, alipeleka mahakamani mashahidi watano na vielelezo 3 ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo kwa kukusudia.

Aidha, Jaji Mnyukwa alisema siku ya tukio hilo mshtakiwa huyo alimvamia Mary akiwa nyumbani kwake majira ya saa 2 usiku na kufa papo hapo kwa madai kuwa ametumwa na baba mkwe wake, Matumizi Anthony kwa ujira wa Sh. 50,000.

Katika kesi hiyo ya mauaji namba 183/2016, upande wa mashtaka uliongozwa na Wakili wa Serikali James Pallangyo na upande wa utetezi wa mshtakiwa ulikuwa ukiongozwa na wakili wa kujitegemea, Mwanzalima Mponeja.

Awali akisoma hati ya mashtaka Karani wa Mahakama hiyo, Renatus Karenge, alidai kuwa Mei 30, mwaka 2013, majira ya saa 2 usiku katika Kijiji cha Kilombero Mkoa wa Geita, mshtakiwa alimuua kwa kukusudia Mary kwa kumcharanga kwa mapanga sehemu mbalimbali za mwili na kufariki papo hapo.

# Tisa wafa ajalini Iringa

**Na Godwin Fransis**

WATU tisa wamefariki dunia na wengine watatu kujeruhiwa kwenye ajali ya gari inayobeba magazeti kwenda mkoani Mbeya.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa, Dk. Iddy Omary, alithibitisha kupokea maiti tisa na kwamba ndugu, jamaa na marafiki wanajitokeza kutambua miili hiyo.

"Tumepokea maiti tisa katika hospitali yetu, zinazoendelea kutambuliwa na kuchukuliwa wakiwamo madereva wawili," alisema.

Aidha, taarifa zinaeleza kuwa majeruhi watatu wanaendelea na matibabu katika Hospitali ya Ilula, wilayani Kilolo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa,

ACP Allan Bukumbi, alithibitisha kutokea kwa ajili hiyo iliyohusisha gari lenye namba za usajili T 249 DWT iliyotokea kijiji cha Mahenge wilayani Kilolo mkoani Iringa juzi majira ya saa 10 alfajiri.

Kamanda Bukumbi alisema gari hilo lilikuwa likitokea Dar es Salaam kuelekea mkoani Mbeya na kwamba chanzo cha ajali hiyo ni mwendo kasi, hivyo dereva akiwa kwenye kona kushindwa kulimudu na kupinduka mara kadhaa.

Aidha, Kamanda Bukumbi alitoa raia kwa madereva kuwa makini barabarani na kuzingatia sheria za usalama barabarani.


## BILO STAR DEBT COLLECTOR CO. LTD

WE ARE DEALING WITH DEBT COLLECTION AND PROPERTY AUCTIONS
(MABINGWA WA KUKUSANYA MADENI SUGU)

### NOTISI YA SIKU (14) NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na mteja wetu BCOM07 LIMITED kuwa mdaiwa tajwa hapo chini unatakiwa kulipa deni unalodaiwa na mteja wetu. Kwamba unatakiwa kulipa deni hilo ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili.Pia tumeelekezwa kuwa ukishindwa kulipa deni hilo ndani ya siku 14 tutauza kwa mnada wa hadhara mali iliyowekwa dhamana ambayo ni kama zifuatavyo;

| JINA LA MDAIWA | DHAMANA | MAELEZO YA DHAMANA | ENEO LA MNADA | TAREHE YA MNADA NA MUDA |
|---|---|---|---|---|
| **EDGAR STEPHEN KIPONDA** | GARI | • T 927 CGH NISSAN PATROL | Ghala la BILO STAR lililopo Mbezi Beach | Tarehe 29/12/2021 kuanzia saa nne asubuhi kuendelea |

**MAELEZO YA GARI:** Lina hati halali (KADI HALISI)

**MASHARTI YA MNADA.**

Mnunuzi atakayefanikiwa gari husika atalazimika kulipa 25% papohapo, na kiasi kilichobaki 75% atatakiwa kulipa ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya mnada. Akishindwa kulipa 25% aliyolipa haitarudishwa na mnada utarudiwa tena.

**NB:**

NDUGU MTEJA UNARUHUSIWA KUJA KUKAGUA GARI HUSIKA KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI. MUDA WA UKAGUZI NI KUANZIA SAA 04:00 ASUBUHI HADI SAA 11:00 JIONI SIKU ZA KAZI NA SIKU YA JUMAMOSI NI KUANZIA SAA 04:00 ASUBUHI HADI SAA 06:30 MCHANA.

**KWA MAELEZO ZAIDI**

**Fika ofisi zetu zilizopo Mbezi Beach au wasiliana nasi kwa simu namba 0716 943424, 0719 206984,bilostarcompany@gmail.com.S.L.P 16095, DAR ES SALAAM.**

RIPOTI MAALUM

## MIAKA 60 YA UHURU

# Ijue misukosuko Baraza la Mitihani na mafanikio yake

- Mitihani ilikuwa inachapishwa UDSM
- Vyeti waliofaulu vilitoka nje ya nchi

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya wakoloni kusema isingewezekana Tanzania kuanzisha Baraza la Mitihani kutokana na uhaba wa watahini na gharama kubwa za uendeshaji mabaraza ya mitihani, mwaka 1971 Tanzania ilichukua uamuzi mgumu wa kujitoa kwenye Baraza la Mitihani la Afrika Mashariki na kuanza kuendesha mitihani yake kama nchi huru.

Uamuzi huo kujitoa kwenye Baraza la Mitihani la Afrika Mashariki ulizingatia mtazamo wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere aliyetaka Tanzania iwe na elimu inayolingana na uhitaji wa jamii, elimu ya kujitegemea. Mwalimu alitaka elimu iendane na uhalisia wa jamii iliyokuwapo baada ya uhuru.

Mnamo mwaka 1973, Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) lilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 21 na marejeo yake kufanyika mwaka 2019. Sheria hii inalipa Baraza la Mitihani jukumu la kuendesha mitihani ya kitaifa na kutoa vyeti kwa watahiniwa waliofaulu mitihani yao.

Kwa mujibu wa Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Charles Msonde, ofisi za baraza kuanzia mwaka 1973 hadi 1981 zilikuwa katika majengo ya Wizara ya Elimu na Utamaduni.

Kutokana na ongezeko la watumishi lililotokana na ongezeko la watahiniwa na shughuli za baraza, mwaka 1981 serikali ilijenga majengo ya baraza eneo la Mikocheni, Dar es Salaam na baraza kuhamia huko.

Dk. Msonde anabainisha kuwa katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania, baraza limepata mafanikio mengi, akidokeza kuwa baada ya kuanzishwa, mitihani ilikuwa inachapwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) hadi mwaka 1983 lilipojenga kiwanda cha chapa na uchapishaji.

Anasema kuwa ili kuongeza ufanisi, serikali za awamu mbalimbali zimeliwezesha baraza kupata mafanikio ikiwamo kununua mashine za uandaaji wa uchapaji, uchapaji wa mitihani na vyeti na ufungaji wa mitihani ya taifa.

Katibu Mtendaji, Dk. Msonde anasema miaka ya nyuma uchapaji wa mitihani na nyaraka zake ulifanywa kwa mashine zenye rangi nyeupe na nyeusi tu (black and white) hali ambayo ilisababisha ugumu kwa wanafunzi kutambua swali wakati wa mitihani kwa kuwa kile walichokuwa wanafundishwa darasani kilikuwa kwenye rangi lakini wakati wa mitihani inakuwa nyeupe na nyeusi tu.

"Kwa jitihada za serikali za awamu mbalimbali, baraza lilifanikiwa kununua mashine ambayo ina uwezo wa kuchapa kwa rangi mitihani na nyaraka mbalimbali.

"Serikali kuanzia awamu ya kwanza hadi ya sita imefanya kazi kubwa sana kuboresha kitengo cha uchapaji. Baada ya kuanzishwa baraza, vyeti vya wahitimu vilikuwa vinatoka nje ya nchi.

"Baada ya kuwezeshwa na serikali, baraza lilinunua mashine za kuchapa na kuweka alama za kiusalama za vyeti na kwa sasa baraza linaweza kutengeneza vyeti vyenye ubora zaidi kulinganisha na vyeti vilivyokuwa vikichapwa nje ya nchi.

"Baraza lilinunua mashine ya kuweka alama mficho za usalama (Hologram) kwenye magamba ya vyeti. Lengo lilikuwa kuondokana na utegemezi wa kuchapa vyeti nje ya nchi," Dk. Msonde anafafanua.

Anaendelea kubainisha kuwa baada ya miaka 60, baraza limepiga hatua kubwa, akikumbusha kuwa awali kazi ya kuhesabu na kufunga mitihani na nyaraka zingine ilifanywa kwa mikono na ilihusisha idadi kubwa ya walimu kutoka nje na ndani ya Baraza la Mitihani pamoja na watumishi wa kada mbalimbali ambao walitumia muda mrefu kukamilisha kazi.

Dk. Msonde anasema kutokana na ununuzi wa mashine mbili za kisasa za kielektroniki (poly wrapping machines), kazi ya kuhesabu na kufunga karatasi za mitihani inafanywa na mashine ambazo zimeongeza kasi na ufanisi.

Dk. Msonde anasema kwamba kwa kuzingatia Tanzania ina sera ya elimu jumuishi, serikali ililiwezesha baraza kununua mashine tano za kuchapa maandishi ya nukta nundu (braille) kwa ajili ya watahiniwa wasioona.

Anasema faida ya mashine hizo ni pamoja na kubadili nakala laini ya mtihani wa kawaida kuwa maandishi ya nukta nundu moja kwa moja pasipo kufanyika uchapaji kama ilivyokuwa awali. Anabainisha kuwa mashine hizo zinarahisisha kazi ya uchapaji na kuongeza usalama wa mitihani.

Katika kipindi cha miaka 60, baraza lilithubutu kuendana na wakati kwa kuunda na kutumia mifumo mbalimbali ya TEHAMA katika utendaji kazi wa kila siku wa baraza na wadau wake. Akifafanua kuhusu mifumo hiyo, Dk. Msonde anasema mifumo ya kusajili wanafunzi wa shule za msingi (PReM) na sekondari (PReMs) kwa kutumia kompyuta imesaidia kuondokana na kero ambazo walimu walikuwa wanapata za kusafiri hadi ofisi za baraza kukabidhi CD zenye takwimu za watahiniwa.

Dk. Msonde anaendelea kufafanua faida za mifumo hiyo kwamba imewezesha wanafunzi kupewa namba ya utambulisho (Unique Identification Number) kuanzia darasa la kwanza hadi ngazi za juu za kielimu, upatikanaji wa takwimu sahihi za wanafunzi kwa shule, kata, halmashauri, mkoa na kitaifa wakati wote.

Pia uhamisho wa wanafunzi kutoka shule moja kwenda nyingine kidigitali na kuondoa usumbufu kwa wazazi kusafiri kwa ajili ya kupeleka nyaraka za uhamisho na kurahisisha uandaaji wa mipango ya maendeleo katika Sekta ya Elimu ya muda mfupi na mrefu na kutoa uamuzi ulio sahihi.

Dk. Msonde anasema baraza limeendelea kuboresha mifumo yake kwa kuunda mfumo wa kupiga picha za wanafunzi waliosajiliwa kwenye mifumo ya kutunza kumbukumbu za usajili wa PReM na PReMS.

Anasema wakuu wa shule za sekondari na msingi hupiga picha watahiniwa wa shule zao kwa ajili ya usajili wa mitihani mbalimbali kwa kutumia simu ya mkononi na taarifa hizo kuingia moja kwa moja kwenye kanzidata ya mifumo ya kutunza kumbukumbu za usajili kwa ajili ya michakato mingine ya kimitihani.

"Mfumo huu umeliwezesha baraza kuokoa fedha kiasi cha Sh. bilioni 2.1 zilizokuwa zikitumika hapo awali kuwalipa wapigapicha mbalimbali nchi nzima waliokuwa wakiteuliwa kwenda kupiga picha wanafunzi shuleni na kuziwasilisha Baraza la Mitihani," anasema.

Mfumo mwingine ambao Dk. Msonde anasema umebadilisha taswira ya baraza ni wa kidigitali wa TSM9.

Itakumbukwa kwa kipindi kirefu walimu walikuwa wanapata shida ya kujaza taarifa za wanafunzi kwa mkono kwenye fomu ya takwimu za wanafunzi (TSM9).

"Kazi hiyo ilitumia muda mwingi na kugharimu pesa nyingi za serikali. Kwa kuzingatia usumbufu waliokuwa wakiupata walimu na kwa lengo la kurahisisha kazi na kupunguza matumizi ya fedha za serikali, baraza liliunda mfumo wa TSM9 unaowezesha upatikanaji wa nakala laini ya TSM9 kidigitali.

"Mfumo ulioundwa na baraza uliwezesha pia kutumwa kwa fomu kidigitali popote zinapohitajika ikiwa ni pamoja na ngazi ya shule, halmashauri na taifa.

"Mfumo huu umeokoa matumizi ya fedha za serikali kiasi cha Sh. billioni 2.3 zilizokuwa zinatumika kuchapa nakala ngumu kila mwaka na kusambazwa mikoani kwa ajili ya kupelekwa kwenye ngazi ya halmashauri na shule," anabainisha.

Anasema baraza pia limeboresha usahihishaji wa Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa kutumia mfumo wa kompyuta kuanzia mwaka 2012.

Anasema mfumo wa TEHAMA wa kusahihisha hapo awali uliundwa na wataalamu wa Kampuni ya Uingereza (DRS) na kugharimu fedha nyingi.

"Wataalamu wa TEHAMA wa Baraza la Mitihani wameweza kuunda mfumo wa TEHAMA wa usahihishaji wa Mtihani wa Darasa la Saba ulioanza kutumika mwaka 2020.

"Kufuatia mafanikio hayo, Baraza la Mitihani limeweza kuondokana na utegemezi wa kutumia mifumo (Software) iliyoundwa na kampuni binafsi ya Uingereza (DRS) ambayo licha ya kugharimu fedha nyingi katika kufanyia maboresho (updates) ya kimfumo, utegemezi ulihatarisha usalama wa takwimu zinazochakatwa," anasema.

Katibu Mtendaji huyo anasisitiza kuwa Watanzania wanapaswa kutembea vifua mbele kwa sababu baraza lao ni mfano wa kuigwa barani Afrika.

"Hii ni kutokana na kupitia uwezeshaji wa serikali, baraza limeunda mfumo wa kuwezesha kufanyika kwa udahili wa wanafunzi kujiunga na vyuo vikuu na vyuo vya kati kwa njia ya mtandao.

"Kwa kutumia wataalamu wake wa TEHAMA wa ndani, baraza liliunda mfumo wezeshi wa TEHAMA (Application Programme Interface-API) ambao unawezesha mifumo ya vyuo vikuu, vyuo ya kati, Tume ya Vyuo Vikuu (TCU), Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) na Sekretarieti ya Ajira kuwasiliana na mfumo wa matokeo ya mitihani ya taifa wa Baraza la Mitihani," anafafanua.

Dk. Msonde anaongeza kwamba mfumo huo umewezesha Watanzania wanaotaka kujiendeleza kielimu kuomba udahili pasi na kuwasilisha vyeti vyao tofauti na kipindi cha nyuma ambapo walilazimika kutembea na vyeti vyao ili kuomba kudahiliwa vyuoni.

Anasema usahihishaji mitihani hufanyika katika vituo mbalimbali kama vile vyuo vya ualimu, shule za sekondari na taasisi zinginezo.

Katibu Mtendaji huyo anasema ili kupunguza mwingiliano wa kazi kati ya baraza na taasisi zinazotumika kwa ajili ya shughuli ya usahihishaji mitihani, serikali iliwezesha baraza kupata fedha za kujenga kituo cha usahihishaji cha Mbezi Wani, Dar es Salaam ambacho kina uwezo wa kupokea wasahihishaji 900 kwa wakati mmoja.

Kutokana na ongezeko kubwa la wanafunzi wanaoandikishwa lililochangiwa na utekelezaji wa sera ya 'Elimu Bila Malipo', Dk. Msonde anasema baraza limepanga kuendelea kuunda na kuboresha mifumo ya TEHAMA itakayopunguza gharama za uendeshaji mitihani.



Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Charles Msonde.

HABARI KITAIFA

## Wakili Mkuu wa Serikali apingwa kuwasilisha kesi

**Na Hellen Mwango**

KAMPUNI ya Coast Textiles Limited, imeiomba Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam kuzuia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kumwakilisha Mkurugenzi wa Bodi ya Bima ya Amana (DIB) ya Benki Kuu (BoT), Isack Kihwili, katika kesi ya kukazia hukumu ya malipo ya Sh. bilioni 145.

Kupitia Wakili Joseph Rutabingwa, kampuni hiyo jana iliwasilisha maombi hayo mbele ya Jaji Amir Mruma kwamba ana shaka iwapo Wakili Mkuu wa Serikali anaweza kuiwakilisha Benki ya FBME ambayo ilichukuliwa na Benki Kuu baada ya kufilisiwa, kutokana na kukataa kufanya hivyo katika maombi mengine kadhaa yanayohusu mwenendo wa kesi.

Pia wakili huyo alidai kuwa suala la uwakilishi liliibuka tena katika ombi lililowasilishwa na benki ikitaka kuongezewa muda wa kukata rufani katika Mahakama ya Rufani, lakini Wakili Mkuu wa Serikali alisema asingeweza kutetea benki hiyo na Shirika Hodhi la Biashara la Consolidate.

Alidai kuwa sababu iliyowasilishwa na Wakili Mwandamizi wa Serikali, Abubarkar Mlisha, kutoka ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwamba Benki ya FBME ilikuwa benki binafsi isiyohusisha maslahi ya umma na DIB ili200letwa kwenye kesi hiyo kwa sababu ya mchakato wa kufilisiwa.

"Wakili wa serikali aliiambia mahakama kwamba DIB inapaswa kusimama yenyewe ili waweze kufika mahakamani. Kufuatia hilo, wito mpya ulitolewa kwa DIB na maombi waliyowasilisha yalikataliwa walipokosa kufika," aliwasilisha hoja Rutabingwa.

Kadhalika, wakili huyo alidai kuwa DIB ilikuwa ikihudumiwa binafsi katika maombi yaliyofuata ambayo yalisababisha kufunguliwa kwa mwenendo wa kukazia uamuzi wa mahakama. "Kwa hivyo, Wakili Mkuu hawezi kuja wakati huu kuwakilisha DIB katika kesi hizi za utekelezaji wa hukumu ya mahakama."

Katika majibu yake ya ombi hilo, Wakili wa Serikali, Edwin Wediro, aliiambia mahakama kuwa kwa mujibu wa kifungu cha 37 (1) cha Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, DIB ni taasisi ya serikali ambayo mamlaka yake ni kufanya ufilisi wa taasisi za fedha kadri itakavyoongozwa na BoT.

Alidai kuwa DIB iliombwa na BoT kuwa mfilisi wa Benki ya FBME na kwa nafasi "Benki ya FBME ambayo iko chini ya ufilisi iko chini ya DIB, ambayo ni taasisi ya serikali, kwa hivyo, Wakili Mkuu ana mamlaka ya kuwawakilisha," alidai.

# Uamuzi mdogo kesi ya Mbowe leo

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi leo inatarajia kutoa uamuzi wa kupokea au kukataa kupokea maelezo ya onyo ya mshtakiwa Mohammed Ling'wenya yaliyopingwa kutokana na madai ya kwamba mshtakiwa huyo aliteswa.

Mshtakiwa anadai alilazimishwa kusaini karatasi na hakuwahi kufikishwa Kituo Kikuu cha Polisi Dar es Salaam kama inavyodaiwa na upande wa Jamhuri.

Mahakama mbele ya Jaji Joachim Tiganga inatarajia kutoa uamuzi leo baada ya kupitia hoja za pande zote mbili pamoja na ushahidi wa mashahidi wanne wa Jamhuri na mashahidi watatu wa upande wa utetezi.

Upande wa Jamhuri mashahidi walikuwa SP Jumanne, Koplo Goodluck, Koplo Msemwa na Mkuu wa Kituo cha Polisi Tazara, Inspekta Lugawa Maulid.

Upande wa utetezi mashahidi ni Komandoo Gabriel Mhina, mshtakiwa Mohammed Ling'wenya na Mwenyekiti wa Baraza la Vijana CHADEMA, Lembrus Mchome.

Shahidi wa mwisho wa upande wa utetezi, Komandoo Gabriel Mhina alidai katika ushahidi wake kwamba polisi walimsulubu na kumpiga kwa saa tatu wakitaka aeleze ana uhusiano gani na Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, alipokataa kuwa na uhusiano naye, aliteswa zaidi.

Shahidi huyo watatu alikuwa mshtakiwa kwenye kesi hiyo ya ugaidi akaachiwa baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuwasilisha hati ya kuwaondoa kwenye kesi pamoja na wenzake wawili Julai 27, mwaka huu.

Alidai Septemba 19, mwaka 2020, alipigiwa simu na rafiki yake anayeitwa Dida wakaangalie mpira Oxygen Pub maeneo ya Makokora mkoani Tabora.

Anadai akiwa eneo hilo ghafla alikamatwa na askari wa kikosi maalum, mmoja alimtolea pisto na kumfahamisha anahitajika kwa RCO.

"Wakati nasubiri kuonana na RCO walinipeleka ndani ya kituo nyuma, waliniuliza kesho kuna tukio gani, nikasema kuna ujio wa Rais Magufuli anakuja kufanya kampeni.

"Kule nyuma walinihoji nina uhusiano gani na Mheshimiwa Mbowe huku wakinipiga vibaya kila sehemu ya mwili wangu, walinipiga kwa kutumia fimbo, ngumi katika taya na mateke.

"Alikuwa Goodluck, kiongozi wao alikuwa afande Jumanne, kulikuwa na Minja na afande Aziz, mmoja simkumbuki.

"Nilipigwa kwa saa tatu, nilipokuwa nakataa kuwa na uhusiano na Mbowe walinipiga zaidi, wakanipeleka Kituo cha Polisi cha Reli Tabora maana hali yangu ilikuwa mbaya," alidai Mhina.

Shahidi anadai walimuuliza kuhusu mshtakiwa wa tatu Mohammed Ling'wenya kama anamfahamu, alikiri anamfahamu, aliwahi kufanya kazi naye Kikosi cha Makomandoo, 92 KJ Ngerengere na alipotoka kazini alikuwa rafiki yake wa karibu.

Anadai alipelekwa Kituo cha Polisi Nzega na walipotoka Nzega walifikishwa Kituo cha Polisi Tazara akiwa na Malema, askari walimfahamisha palikuwa Tazara.

Shahidi anadai alifika Tazara Septemba 23, 2020, akakaa siku mbili ilipofika Septemba 25 alifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu na kutuhumiwa kwa ugaidi.

Anadai akiwa Tazara mahojiano yalikuwa yakifanyika juu kulikuwa na chumba, anadai Malema alihojiwa na Inspekta Mahita Omari na yeye alihojiwa na SP Jumanne.

Anadai aliambiwa ataunganishwa na wenzake kwenye kesi ya ugaidi namba 63/2020, akiwa Tazara alikuwa anakunywa maji tu, chakula alikula Septemba 25 gerezani baada ya kutoka mahakamani.

"Julai 27, mwaka huu, tulipofika mahakamani Hakimu Thomas Simba alisema serikali haina nia ya kuendelea na shauri letu nikaachiwa mimi, Kaaya na Khalid.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Adamu Kasekwa, Ling'wenya na Halfani Bwire ambao wanatuhumiwa kwa mashtaka sita yakiwamo kula njama kufanya vitendo vya kigaidi kati ya Mei mosi na Agosti 5, mwaka 2020.

Washtakiwa wanadaiwa kutenda makosa hayo maeneo ya Dar ea Salaam, Arusha, Morogoro, Mbeya na Mwanza na Kilimanjaro.




Meneja wa Tigo Kanda ya Pwani Kaskazini, Robert Kaluswa (kushoto), akikabidhi funguo ya pikipiki kwa Ezra Mwaikambo baada ya kuibuka mshindi wa pili wa pikipiki katika promosheni ya Wagiftishe Gift juu ya Gift, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Nondo za mamilioni zanaswa zikisafirishwa bila risiti za EFD

**Na Mwandishi Wetu,** MKURANGA

MAMLAKA ya Mapato (TRA) imefanya ukaguzi wa risiti za elektroniki (EFD) katika malori ya mizigo yanayoelekea mikoa ya kusini eneo la Mwandege wilayani Mkuranga mkoani Pwani, ikikamata malori 21 yaliyokutwa na makosa ya kutokuwa na risiti hizo. Mbali na kutokuwa na risiti hizo, watumishi wa mamlaka hiyo pia wamebaini wamiliki wa malori hayo kutokuwa na risiti ya gharama ya usafirishaji mzigo, jambo ambalo ni kinyume cha sheria kwa kuwa usafirishaji ni biashara kama zilivyo biashara zingine.

Meneja Msaidizi wa TRA Mkoa wa Pwani, Chipa Chikwekwe, aliiambia Nipashe jana kuwa wamegundua kutokutoa risiti ni tatizo kubwa kwa baadhi ya wamiliki wa malori, akiwataka kuzingatia utaratibu huo wa kisheria ili kuepuka faini na adhabu zisizo za lazima.

Alibainisha kuwa katika kituo hicho cha Mkuranga, moja ya malori yaliyokamatwa juzi na maofisa wa TRA ni lenye namba T310CFK la kiwanda cha M/s Hangjin Steel LTD, lililokuwa linasafirisha nondo kwa ajili ya Kampuni ya M/s Kayanja Stores LTD ambaye mmiliki wake ni Dickson Kahwa.

Meneja huyo alisema lori hilo lilikamatwa baada ya kugundulika kuwa mzigo huo wa nondo haukuwa na risiti EFD na kuchukuliwa hatua za kisheria ambapo ametakiwa kulipa faini ya Sh. milioni 1.5 kwa kutokudai risiti.

"Pia muuzaji amekubali kutoa risiti ya thamani ya mzigo Sh. milioni 54 ikiwa na VAT (Kodi ya Ongezeko ka Thamani) Sh. milioni 8.2. Output Tax itawekwa kwenye ritani yake ya VAT.

"Vilevile muuzaji ametakiwa kulipa faini ya Sh. milioni 4.5 kwa kosa la kutokutoa risiti ya EFD. Sambamba na hayo, muuzaji amekubali kulipa fini ya Sh. milioni 16, yaani mara mbili ya kodi ya VAT ambayo aliikwepa kwa kutokutoa risiti ya EFD," alibainisha.

Pia alisema mfanyabiashara wa lori wa nondo, Said Seleman, ameshtakiwa kwa kosa la kutokuwa na risiti kwa madai alisahau alikochukulia mzigo.

Hata hivyo, Chikwekwe alisema mfanyabiashara huyo alikiri kwamba TRA inafanya utaratibu mzuri wa kukagua risiti kwa kuwa inawakumbusha kuzingatia sheria, hivyo akaomba ukaguzi huo uwe endelevu ili wawe na amani wanapokuwa barabarani. Alibainisha kuwa wamiliki wa malori wamekuwa wakivizia nyakati za usiku kupitisha mizigo, wakiamini kwamba muda huo maofisa wa TRA hawako kazini.

Kuanzia mwaka 2010 mfumo wa EFD ulipoanzishwa kwa wafanyabiashara waliosajiliwa kwa kodi ya VAT na mwaka 2014 kwa wafanyabiashara wasio wa VAT, TRA imeendelea kusisitiza matumizi ya mashine za EFD kwa kuwataka watoa huduma kutoa risiti pindi wanapofanya mauzo na wanunuzi kudai risiti pindi wanaponunua bidhaa kwa lengo la kufanya makadirio ya kodi yaliyo sahihi na pia kumwezesha mtoa huduma kujua mwenendo wa biashara yake.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kwa haya Jeshi la Polisi lijitafakari

**JUZI** Rais Samia Suluhu Hassan, alieleza madhila aliyokumbana nayo wakati akiwa raia na mtumishi wa kawaida serikalini kwa kunyanyaswa na askari polisi.

Rais alitumia mifano yake halisi kuonyesha Jeshi la Polisi lenye wajibu wa kulinda raia na mali zao, limegeuka kuwa maumivu kwa wananchi wengi kwa kutumia nguvu kuumiza wasio na hatia.

Hii ni mara ya pili ndani ya mwaka huu kwa Rais kufikisha ujumbe wenye kuwasilisha maumivu ya wengi dhidi ya matendo yanayofanywa na baadhi ya polisi ambao sio waadilifu.

Rais bila kumung'unya maneno alisema rushwa, matumizi ya nguvu kuliko akili, kuonea watu, kubambikia kesi, kuwapiga, kuwatesa ni miongoni mwa mambo yanayolichafua jeshi hilo na kutaka kufanyike maboresho makubwa ili kurudisha hadhi.

Mifano aliyoitoa Rais Samia ni halisi ya maisha ya watu ya kila siku, na hapo angalau baadhi ya sehemu walimgundua kuwa ni kiongozi wa serikali makali yakapungua, na kama angekuwa raia wa kawaida hali ingekuwa tofauti kabisa.

Mfano aliotumia Rais wa taa ya gari kutowaka hutokea bila dereva au mmiliki kujua, lakini kutokufanyakazi kwa kifaa cha kurusha maji ya kusafishia kioo, lakini unapokamatwa na polisi huwa ni kutozwa faini au umpe rushwa na wakati mwingine hataki kukusikiliza.

Tunatambua kuwa wapo polisi waadilifu wanaofanya kazi nzuri na wengine wamejitoa kusaidia na kuokoa maisha ya wengi bila kujali hali yao na mazingira yoyote na tunaamini wanaochafua jeshi hilo ni wachache ambao wametanguliza tamaa mbele.

Tunathamini na kutambua kazi wanayoifanya ya kupambana na uhalifu wa aina mbalimbali na wapo waliopoteza maisha wakati wakipambana na uhalifu, yote hiyo ni katika kulinda raia na mali zao.

Imekuwa kawaida watu kubambikiwa kesi kubwa kubwa kama za jinai huku wengine wakisota rumande za vituo vya polisi bila kufikishwa mahakamani ndani ya saa 24 kwa mujibu wa sheria wala dhamana ambayo ni haki ya mtuhumiwa.

Wachache hawa wamegeuka kuwa maumivu kwa wengi hasa kutumia nguvu bila akili, kutesa watuhumiwa ambao wengine hufariki na kupata ulemavu wa kudumu, pia kupokea rushwa na baadhi kudaiwa kujihusisha na uhalifu wa aina mbalimbali kama wizi wa mali za raia na mwingine.


Barabarani nako ni kilio kwa kuwa wananchi hubambikiwa makosa kwa kuonyeshwa kamera za uongo kuwa wametembea kwa mwendokasi na wakati mwingine kutakiwa kutoa rushwa kwa lazima au aandikiwe faini au wengine kuandikiwa faini kwa adhabu ambazo hawajatenda.

Mathalani, kwa sasa kuna mchezo wa kuonea madereva kwenye mistari ya pundamilia, yaani askari wanajificha au kusimama mbele ya mistari kuangalia gari ambalo halijasisimama hata kama hakuna mtembea kwa miguu, gari linatakiwa kusimama.

Wakati mwingine dereva amesimama kwa muda kupisha watembea kwa miguu, lakini anapoondoa gari anasimamishwa kwa kuwa mtembea kwa miguu kajitokeza anataka kupita.

Eneo jingine ni kwenye taa ambazo wakati mwingine hazifanyi kazi hutumika kama kichaka kwamba dereva anaambiwa amevuka kwenye taa nyekundu wakati kiuhalisia sio kweli, na ndiyo maana tunasema ifike mahali kuwe na kamera kwenye taa ambazo zitapiga picha kuonyesha uhalisia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Tusikwepe kusema ni Uhuru wa Tanganyika

Na Askofu Mwamalanga

**KAMATI** ya Kitaifa ya Pamoja ya Maaskofu na Mashehe ya Maadili Amani na Haki za Binadamu kwa Jamii ya Madhehebu ya Dini, haijafurahishwa na matangazo ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika ya Desemba 9.

Maadhimisho hayo yalikuwa yanakwepa na kuacha kuitaji Tanganyika, badala yake yalikuwa yanaishia na maadhimisho ya miaka 60 ya uhuru.

Sisi viongozi wa dini nchini tumeshangazwa na kulikwepa jina hilo tukiamini huenda ni jambo linalofanywa kwa makusudi kwa lengo la kuwafanya wananchi wasifahamu ukweli wa uhuru na kuaminisha kuwa Tanzania ndiyo ilipata uhuru.

Viongozi wa dini tunauchukulia kuwa ni upotoshaji mkubwa na wa makusudi wenye lengo la kuongeza viraka kwenye Muungano wetu ambao unatokana na Tanganyika huru na Zanzibar huru iliyozaliwa na Mapinduzi ya 1964, ndiyo maana kila upande kuna sherehe za uhuru.

Ni kama utamaduni ambao umekuwa nguvu ya kuimarisha Muungano ambao ni ushirikiano unaoletwa na Zanzibar na Tanganyika kuungana.

Kujaribu kuondoa Uhuru wa Tanganyika kunaweza kuhusishwa na kukwepa kuyataja Mapinduzi ya Zanzibar maana yake ni kuiondolea nyumba ya Tanzania Muungano nguzo zake na kujaribu kupotosha historia mahsusi.

Kukwepa kusema Uhuru wa Tanganyika, kunafanyika mbele ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan.

Ni vyema Wizara ya Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ijinyooshee kidole kwa kuchukua hatua kujifungia yenyewe kama ambavyo imekuwa ikifungia vyombo vingine vya habari yakiwamo magazeti na radio ili kulinda maadili ya uongozi na kuitii sheria bila shuruti, ambacho ndicho kioo cha vyombo vyote vya habari nchini.

**Kujaribu kuondoa Uhuru wa Tanganyika kunaweza kuhusishwa na kukwepa kuyataja Mapinduzi ya Zanzibar maana yake ni kuiondolea nyumba ya Tanzania Muungano nguzo zake na kujaribu kupotosha historia mahsusi.**

Viongozi wa dini nchi walitegemea kauli za Uhuru wa Tanganyika ziwe za kupinga dhuluma, ukandamizaji wa haki za watu, matumizi mabaya ya madaraka, ufisadi, ubambikizaji kesi watu wakiwamo wanasiasa na kuondokana na sheria zinazokandamiza raia kila uchao na kuwalinda wachache kero ambayo Watanzania wanaipigia kelele kila siku.

Aidha, viongozi wa dini tunaona ni sherehe hizi za Uhuru wa Tanganyika ziwe muafaka wa maridhiano kwa wanasiasa, kusameheana na kuondokana na kuvichukia vyama halali vya kisiasa na viongozi wake.

Tunapenda kusema kuwa hii haipendezi tumegundua ni chanzo kikubwa cha watu kufanya ufisadi unaofanywa na kikundi kidogo cha watu kukumbatia keki yote huku mamilioni ya Watanzania wakiishia kugawana umaskini.

Sherehe za Uhuru wa Tanganyika tungependa ziwe mtetezi wa wakulima kutokana na bei kubwa ya kutisha ya mbolea ambayo sasa ni zaidi ya Shilingi 100,000 kwa mfuo wa kilo 50.

Ni wakati wa kuangalia tatizo la mbolea linatatuliwaje kwasababu kuyumba kwa kilimo kutasababisha au kutakaribisha njaa kutokana na wakulima wa chakula wa mikoa ya Mbeya, Songwe, Iringa, Rukwa na Katavi kukwamishwa na bei ya mbolea ya kupandia na kukuzia.

Tunaiomba serikali kuacha kuziba masikio kama ilivyoziba masikio kwenye mbolea, kuendelea kufanya hivyo ni kuwaondolea wananchi uhuru wa maendeleo ndani ya miaka 60, hayo yote ndiyo yanayochochea uwepo wa katiba mpya.

Katiba hiyo ndiyo itakayoruhusu uhuru wa mawazo ya raia wote wa Bara na Visiwani.

HABARI KITAIFA

# Kasi uharibifu ardhi ya kilimo ilivyowashtua wataalamu

**Na Salome Kitomari**

KASI ya uharibifu wa udongo maeneo ya kilimo imewashtua wataalamu wa miti na misitu kutoka nchi 11 za Afrika, waliokusanyika kujadili nini cha kufanya kutunza rasilimali hiyo, ili kupunguza na kukabili mabadiliko ya tabianchi.

Akizungumza hivi karibuni wakati wa uwasilishaji mada mbalimbali za mabadiliko ya tabianchi, hali ilivyo kwenye nchi husika, hatua zilizochukuliwa na utekelezaji wa makubaliano ya kitaifa na kimataifa, Katibu Mtendaji wa Jukwaa la Misitu Afrika (AFF), Prof. Godwin Kowero, alisema wakulima wamejikuta kwenye wakati mgumu kuendeleza kilimo na madhara yatakuwa kwa watu wote.

Alisema kwa sasa mvua zinachelewa na zinaponyesha kwa wingi, ni za uharibifu kwa kuwa udongo wenye rutuba unazolewa kutoka milima na kusafirishwa kwenda mtoni, ziwani na baharini inayobaki inakuwa haina rutuba.

"Kuna utafiti ulifanyika Ziwa Victoria ukaonyesha sakafu yake imejaa plastiki. udongo umeharibika sana kwa kuwa ule wenye rutuba umezolewa kwenda tambarare na sasa kuna kazi kubwa ya kurudisha udongo ili ufae kwa kilimo," alisema.

Alisema Afrika imekuwa nyuma kupata nafasi kwenye majukwaa ya kimataifa yenye kufanya maamuzi mbalimbali, hasa kutokana na kubadilibadili mwakilishi wa masuala ya nchi kwenye jambo fulani.

"Afrika inakosa maamuzi ya pamoja kwenye mambo mbalimbali kwamba wanapokwenda kwenye jumuiya za kimataifa wawe na msimamo mmoja na lugha moja, lakini imekuwa kawaida kila mmoja anakwenda na lake kiasi kwamba ni kama wanashindana,"alisema.

Mathalani alisema Cuba mwakilishi wake kwenye masuala ya mazingira amekuwa mmoja kwa miaka 20, ambaye ana uelewa mkubwa anajua namna ya kupigania nafasi ya nchi yake kwenye majukwaa mbalimbali, lakini kwa nchi za Afrika kila wakati anabadilika kwa kadri ya waziri au kiongozi wa nchi anavyobadilika jambo linalokosesha mwendelezo. Naye Mkufunzi wa Misitu, Mazingira na Sayansi ya Jiografia wa Chuo Kikuu cha Makerere nchini Uganda, Dk. Michael Mbogga, alisema nchi za Afrika zinahitaji sera zenye kutambua kazi za kisayansi zenye ushahidi wa kusaidia kukabili mabadiliko ya tabianchi.

Alisema baadhi ya sera na sheria za nchi ni za zamani hazijalibeba suala la mabadiliko ya tabianchi kama moja ya mambo muhimu kwa kuwa ni jipya, na kwamba ni muhimu likabebwa kuwa miongoni mwa mambo ya msisitizo.

Naye Mkuu wa Chuo cha Misitu, Wanyamapori na Utalii cha Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Prof. Suzana Augustino, alisema kumekuwa na madai kwamba uvunaji mkaa ndiyo sababu kubwa ya kuharibu misitu na miti, lakini hiyo ni sehemu ndogo sana.

"Kuna utafiti ulifanyika ukaonyesha tunaweza kuwa na uvunaji mkaa endelevu kwa kuwa miti inayoweza kuvunwa na kupandwa mingine ambayo huota kwa haraka, wananchi wanaweza kukubaliana kuvuna kwa awamu huku wanaotesha kuliko hali ilivyosasa wanavuna ovyo," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Shirika lisilo la kiserikali la Comparatively for Tanzania Elites Community Organization, Mussa Mussa, alisema ni muhimu serikali ikapunguza bei ya gesi na umeme ili kuwawezesha wananchi wa kawaida kumudu nishati hiyo.

"Ni muhimu pia kukafanyika utafiti kuonyesha ni kwa kiasi gani mkaa unachangia uharibifu wa mazingira, wananchi hawajakataa kuacha matumizi ya mkaa, lakini wanaacha wanatumia nishati gani wakati mbadala zilizopo ni gharama kubwa?" Alihoji.

Naye Mkufunzi wa Idara ya bidhaa za misitu na uzalishaji wa Chuo Kikuu cha Ibadan, Nigeria, Dk. Adejoke Akinyele, alisema kasi ya uharibifu wa ardhi ni kubwa kiasi kwamba wakulima hawaoni thamani ya ardhi kwa kuwa hawavuni mazao na sasa wanakwenda kwenye maeneo machache yaliyohifadhiwa ya misitu kufanya shughuli zao.

Alisema misitu inasaidia kunyonya hewa ukaa inayosambaa angani na ndiyo maana kumekuwa na msisitizo wa kuifanya jamii kutunza miti na misitu kwa kuwa itasaidia kutunza ardhi ambayo wananchi wataitumia kwa shughuli za uzalishaji.



Mwezeshaji wa mafunzo kuhusu bajeti ya mrengo wa kijinsia, Jovita Mlay kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), akiendesha mafunzo hayo kwa viongozi wa idara mbalimbali za Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Wakuu wa shule sekondari kuketi na Rais Samia

**Na Mwandishi Wetu**

WAKUU wa shule za sekondari watajadili vikwazo na mafanikio watapokutana mkoani Dar es Salaam.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Wakuu wa Shule za Sekondari (TAHOSSA), Titus Jumanne, alisema mkutano huo unatarajiwa kuhudhuriwa na walimu 5,000.

Alisema mkutano huo wa 16 utakaoanza kesho na kufunguliwa na Rais Samia Sulihu Hassan, unawaleta pamoja wakuu hao wa shule ili kubadilishana mawazo kuhusu vikwazo na mafanikio na utekelezaji wa sera na mipango inayotolewa na serikali.

Alisema kwenye mkutano huo kutakuwa na tukio la utoaji wa zawadi mbalimbali kwa shule, walimu na wanafunzi waliofanya vizuri kitaaluma.

Alisema mkutano huo utajadili mafanikio mbalimbali ya elimu yaliyopatikana katika awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan ikiwamo ujenzi wa shule na maelfu ya madarasa mapya.

Aliishukuru serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule moja ya wasichana kwa mikoa 10, hali ambayo alisema itasaidia kuwapunguzia adha ya kusafiri umbali mrefu watoto wa kike kwenda shule.

"Hiki ni kipindi cha kushangilia mafanikio ya elimu katika kuadhimisha miaka 60 ya Uhuru, Rais Samia atakutana na wakuu wa shule nchi nzima na kuzungumza nao masuala mbalimbali yanayohusu elimu na kuwapa mwelekeo wake kwenye sekta hiyo," alisema Jumanne.

Alishukuru serikali kwa kupeleka Sh. bilioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari mpya zipatazo 214 ambazo zitajengwa kwenye majimbo yote nchini.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard Akwilapo, alithibitisha kuwa Rais Samia atakuwa mgeni rasmi kwenye mkutano huo.

# Mfanyabiashara aachiwa huru kesi ya mauaji

**Na Samson Chacha, TARIME**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Musoma, imemwachia huru mfanyabiashara wa duka la vifaa vya ujenzi mjini Tarime, Lucas Soteri aliyekuwa akikabiliwa na kesi ya mauaji.

Soteri alishtakiwa kwa mauaji ya Wankuru Makenge, aliyetuhumiwa kuweka mawe barabarani Kijiji cha Buriba, Kata ya Sirari kwa lengo la kufanya uhalifu.

Uamuzi wa mahakama hiyo umetokana na upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha makosa hayo kutokana na mkanganyiko kwenye ushahidi.

Akisoma hukumu hiyo, Jaji Mfawidhi wa mahakama hiyo, John Kahyoza, alisema kesi yoyote ya jinai ikiwamo za mauaji, ili mtu aweze kuhukumiwa ni lazima kuwapo ushahidi unaojitosheleza.

Alisema shahidi wa kwanza, Selvester Geteba, alidai mahakamani Oktoba 9, mwaka 2014, majira ya saa nne, walikuwa na marehemu Wankuru na mwenzake aliyemtaja kwa jina moja Mustapher wakiwa barabarani karibu na mnara wa simu wakichaji simu.

Jaji Kahyoza, alisema shahidi huyo alieleza mahakama kuwa wakiwa barabarani alifika mfanyabiashara wa mifugo na mkulima Msabi Magasi, wakiwa ndani ya gari dogo lenye namba za usajili T 166 AWE.

Hata hivyo, alisema hakuweza kumtambua dereva wa gari, lakini Msabi alishuka kutaka kuondoa mawe yaliyokuwa barabarani, lakini dereva aliamuru warudi nyuma na kutokana na mawe hayo ilitafsiriwa wametaka kufanya uhalifu ndipo dereva alifyatua risasi hewani.

Alidai watu hao walirejesha mawe tena barabarani huku wakiwa na silaha za jadi, mapanga na marungu na kuzuka kutoelewana.

Naye shahidi ambaye ni Mganga wa Hospitali ya Wilaya, Benard Makoyo, alidai Oktoba 10, 2014, aliufanyia uchunguzi mwili wa marehemu Wankuru Makenge, mbele ya ndugu wa marehemu, Mwenyekiti wa kitongoji Juma Mokeha na polisi wa upelelezi, ambao ulikutwa na jeraha kutoka kifuani kwenda mgongoni ambalo lilikuwa ni kuchomwa na kitu chenye ncha kali.

Ushahidi huo uliungwa mkono na shahidi wa nne askari polisi kitengo cha upelelezi, Mustapher aliyedai kufika eneo la tukio wakiwa na Mwenyekiti huyo wa kitongoji, Mokeha, ndugu wa marehemu na wananchi na kukuta mwili wa marehemu, kando kukiwa na mawe na walipomuhoji mlinzi wa mnara huo alidai ilisikika milio ya risasi na kuna mtu alikuwa na mshale.

Alisema mashahidi hao kwa nyakati tofauti walidai jeraha alilokutwa nalo marehemu siyo la risasi bali kitu chenye ncha kali, huku anayejatwa ni mtu aliyetambulika kwa jina la Ten ten au Soteri, na kwamba mahakama haiwezi kutoa adhabu kwa ushahidi wa mashataka ambao haujathibitishwa.

Kwa mujibu wa jaji huyo, mashahidi wa upande wa utetezi wamejichanganya kwa kuwa marehemu na wenzake walikuwa na nia ya kutenda uhalifu ndiyo maana waliweka mawe barabarani.

Aidha, alisema kutokana na hali hiyo mahakama imemwachia huru mshtakiwa huyo.

# Kinondoni yatakiwa kutenga bajeti ya mrengo wa kijinsia

**Na Sabato Kasika**

MANISPAA ya Kinondoni mkoani Dar es Salaam, imeshauriwa kutenga bajeti yenye mrengo wa kijinsia, yenye mahitaji ya kimkakati inayowezesha safari ya maendeleo ambayo kila mtu anatakiwa kuyapata.

Bajeti hiyo pia inatakiwa kuakisi jamii ili kujikwamua kiuchumi, kifikra, kiuongozi na inayomzindua mwanamke na mwanaume na kumpa fursa za mikopo hadi ufikiaji wa rasilimali.

Hayo yalisemwa, jijini Dar es Salaam jana na mwezeshaji wa mafunzo kuhusu umuhimu wa bajeti ya mrengo wa kijinsia, Jovita Mlay, kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).

Mafunzo hayo yalitolewa kwa wakuu wa idara mbalimbali za manispaa hiyo, ili kwamba bajeti yao ijayo izingatie mrengo wa kijinsia ili kunufaisha wanawake, ambao alidai kuwa wameachwa nyuma.

"Mnapoandaa bajeti yenu ijayo, zingatieni mrengo wa kijinsia hasa yenye inayokwenda sambamba na mahitaji ya kimkakati na inayowezesha safari ya maendeleo ambayo kila mtu anatakiwa kuyapata," alisema Jovita.

Alifafanua wakati wa uandaaji wa bajeti, wanawake na wanaume wanaalikwa na kuibua fursa na vikwazo vya maendeleo kuanzia ngazi ya kijiji na kata, huku taarifa mapato na matumizi zikisomwa na kuwekwa katika ubao wa matangazo.

"Idadi ya wanawake wanaoshiriki katika mikutano ya uandaaji wa bajeti, wanatakiwa kufikia asilimia 30, na kwamba mambo yanayoibuliwa na wanawake yanapata nafasi ya kuingizwa kwenye bajeti," alisema.

Ofisa Mipango wa manispaa hiyo, Febronia Luyagaza, alisema wanatekeleza bajeti kulingana na vipaumbele vilivyoelekezwa na serikali, na kwamba kadri hali itakavyoruhusu wataendelea kuzingatia bajeti ya mrengo wa kijinsia.

"Lakini tunashukuru kwa mafunzo haya, kwani yana umuhimu mkubwa, nasi tumeyapokea tutayafanyia kazi, ila mfumo wa bajeti zetu ndivyo ulivyo, kwamba tunafuata vipaumbele vilivyoelekezwa na serikali,"alisema Luyagaza.

Mkuu wa Idara ya Elimu wa manispaa hiyo, Theresia Kyara, aliishauri TGNP kupanua kazi zake na kwenda kwenye matukio na kutoa elimu, ili kusaidia na serikali kupambana na vitendo visivyofaa ndani ya jamii.

"Ninashauri mafunzo haya yasiishie kwetu, bali TGNP mwangalie uwezekano wa kupanua shughuli zetu, badala ya kuitisha mafunzo kama haya, mjaribu kwenda hata kule ambako mnaona kuna shida ili kuelimisha," alisema Kyara.



Wahitimu wa Chuo cha Diplomasia waliotunukiwa Stashahada ya Uzamili katika Kudumisha Amani na Utatuzi wa Migogoro na Menejimenti ya Uhusiano wa Diplomasia, wakiwa pamoja baada ya kutunukiwa vyeti katika mahafali yaliyofanyika jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Wateja M-Pesa wapata gawio la bil. 4.9/-

**Na Elizabeth Zaya**

KAMPUNI ya teknolojia na mawasiliano nchini (VODACOM), imetangaza kutoa Sh.bilioni 4.9 kama gawio kwa wateja wake wa M-Pesa ambao wametumia huduma hiyo kwa kipindi cha robo ya tatu ya mwaka, kuanzia Julai hadi Septemba mwaka huu.

Mkurugenzi wa M-Pesa, Epimack Mbeteni, alisema pesa hiyo ni faida na italipwa kwa wateja wote, mawakala wa rejareja na washirika wengine wa biashara wa M-Pesa ambao watapokea malipo kutokana na huduma ya malipo waliyofanya kupitia simu zao za mkononi.

"Huduma yetu ya pesa kupitia simu za mkononi, M-Pesa, inaendelea kwa mafanikio na ikitoa thamani kwa kijamii na kifedha kwa Watanzania. Tumeona ukuaji mkubwa kwenye jukwaa la M-Pesa na wateja, mawakala, wafanyabiashara na taasisi zinazofanya biashara kufikia karibu Sh.bilioni 100 kila siku. Leo (jana) tunafurahi kushiriki katika utoaji wa gawio la Sh. bilioni kwa wateja wetu zaidi ya milioni 8 kote nchini, "alisema Mbeteni.

"Vodacom Tanzania ina zaidi ya wateja milioni 11 kwenye jukwaa lake la M-Pesa inayomiliki sehemu ya soko ya asilimia 40 kulingana na takwimu za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) za hivi karibuni. Hadi sasa kampuni imelipa Sh.bilioni 167.8 ikiwa ni riba iliyolipwa tangu Julai 2015 na sehemu ya faida kwa kila mteja imehesabiwa kulingana na namna mteja alivyotumia huduma ya M-Pesa, kiwango cha shughuli ambazo wamezifanya kupitia M-Pesa kwa kipindi hicho."

Alisema wameanza kusambaza fedha kwenye akaunti za wateja hao na kwamba ili wapate fedha hizo kuna namba watakiwa kuingiza.

"Tumeanza kusambaza pesa kwenye akaunti za wateja wa M-Pesa na watatumia neno KIASI au AMOUNT kwenda 15300 kwa ujumbe mfupi ili kujua ni kiasi gani cha faida watakachopokea. Baada ya kupokea kiasi kilichotolewa, wateja watatumia pesa hizo kulipia huduma au kufanya matumizi ya aina yeyote wanayojisiki," alisema Mbeteni.

"Tutaendelea kuzingatia ushirikiano wa kimkakati na kudumisha aina anuwai za huduma ambazo hufanya malipo haraka, rahisi na salama kwa wafanyabiashara na watu binafsi."

# NMB kuboresha shule, hospitali mkoani Mbeya

**Na Christina Mwakangale**

BENKI ya NMB imeahidi kushirikiana na Taasisi ya Mbeya Family Group (MFG) kuinua maendeleo kwenye jamii, kwa kuboresha miundombinu kwenye shule na hospitali hususan vyoo, mkoani Mbeya.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki katika taarifa yake iliyosomwa na Mkuu wa Idara ya Bima wa benki hiyo, Martin Massawe, kwenye ufunguzi wa mkutano na uchaguzi mkuu wa viongozi wa taasisi hiyo, uliofanyika mkoani Dar es Salaam.

Alisema kutokana na taasisi hiyo kuonyesha nia na kusaidia jamii, ikiwa ni kati ya malengo ya benki hiyo, watashirikiana na MFG, ili kuhakikisha kunakuwapo vyoo vyenye ubora shuleni na baadhi ya hospitali.

"Benki ya NMB, tunajikita kwenye miradi tofauti na tumekwishatoa Sh. bilioni 10 kusaidia huduma za shule tofauti kwa miezi sita. Kupitia NMB Foundation, tutaanza kukarabati vyoo kwa kushirikiana na MFG," alisema Zaipuna.

"NMB Dunduliza' naamini tutafanikisha huduma ya bima ya afya, huu ni mpango maalumu ulioangalia mamna gani gharama za matibabu zitapungua kwa ambao wanatumia huduma hiyo."

Aliishauri taasisi hiyo kutumia fursa za kiuchumi zilizopo mkoani Mbeya ili kuinua umoja wao na kwamba kuanzishwa kwa SACCOS ya taasisi hiyo, itasaidia kuongeza wigo wa shughuli zao kama kikundi.

Awali, Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Michael Mwangoka, alisema malengo ya taasisi ni kujikwamua kiuchumi na kwamba MFG, inahusisha wazaliwa, wakazi, waliosoma, na waliowahi kuishi mkoani Mbeya, bila kujali itikadi za dini, siasa na ukabila na hadi sasa ina wanachama wapatao 150.

"Lengo la umoja huu ni kufarijiana na kusaidia wakati wa shida na raha pamoja na kusaidia jamii, kugharamia matibabu, kufarijiana katika shida na raha miongoni mwa wanachama, pia kuboresha huduma za kijamii. Tayari Shule ya Msingi Majengo, Mbeya tumefanya ukarabati wa vyoo, uliogharimu Sh. milioni 20 zilizochangwa na wanachama," alisema Mwangoka.

Mwangoka alisema, wamejisajili katika huduma ya bima ya mazishi kupitia Benki ya NMB akisema lengo ni kutoka taasisi hadi kuwa SACCOS na tayari suala hilo limewasilishwa kwa wadau inasubiri utekelezaji.

Mkutano huo umehudhuriwa na wakazi wa Mbeya waishio katika mkoa huo na kutoka mikoa mbalimbali ikiwamo Dar es Salaam, Dodoma na waishio nchi za Malawi, Uingereza na Australia.

Mwenyekiti wa Matukio wa MFG, Rose Mkisi, aliwashukuru wanachama wa taasisi hiyo kutoka ndani na nje ya nchi, kwa kuonyesha ushiriki wao, kwenye mkutano huo ambao hufanyika mara moja kwa mwaka.

HABARI KITAIFA

# Taasisi za fedha zaombwa kusaidia wakulima kahawa

**Restuta Damian,** BUKOBA

TAASISI za Fedha mkoani Kagera zimetakiwa kuangalia namna ya kusaidia wakulima wa kahawa katika kutoa mikopo kuongeza tija na uzalishaji.

Hayo yalisemwa mwisho mwa wiki hii na Mkurugenzi wa Shirika lisilo la kiserikali lenye kujihusisha katika tija na uzalishaji bora wa zao la kahawa mkoani humo, Dafrosa Sanga, wakati akizungumza na wadau wa asasi mbalimbli za fedha ili kumsaidia mkulima kutatua tatizo la upatikanaji wa fedha kwa haraka.

Sanga alisema, lengo la kukutanisha taasisi hizo ni kusaidia mkulima ambaye amekuwa na mahitaji mengi katika kuhudumia shamba kuanzia kwenye upandaji utunzaji hadi mavuno.

Alisema, kumekuwapo na gharama katika usafishaji wa miche ya kahawa kufikisha shambani, upanuzi wa mashamba mapya ikiwa ni kuongeza uzalishaji.

"Hakuna ambapo fedha haitakiwi iwe ni malipo ya mkulima, iwe usafirishaji mazao, utafutaji wa pembejeo maeneo yote hayo yanahitaji fedha," alisema.

Aidha, alisema, shirika hilo limefanya jitihada kufufua mashamba ya kahawa yaliyokaa muda mrefu, uanzishaji wa vitalu vya miche ambayo inapandwa na mkulima kama njia ya kujifunza kilimo bora na cha tija.

"Tumeweza kuanzisha mashamba darasa 200 na kufikia wakulima zaidi ya 10,000 kwa kuwapatia kilimo tija na wingi wa mavuno," alisema Sanga.

Makamu Mwenyekiti Taasisi ya Utafiti wa Kilimo cha Kahawa Tanzania (TACRI) mkoani Kagera, Andrew Paul, alisema, endapo mkulima akipatiwa fedha ana uwezo wa kuwekeza katika kilimo na kupata manufaa.

Alisema, ukosefu wa fedha kwa wakati unafanya mkulima kuuza kahawa kabla ya kukomaa shambani kwani kufanya hivyo ni kutatua mahitaji.

Katibu Tawala (Uchumi na Biashara) mkoani humo, Isaya Tendega, alisema, mkoa una wazalishaji wa mashamba madogo ambao kipato chao ni cha hali ya chini.

# Kipindupindu chaibuka Nkasi

**Na Gurian Adolf,** NKASI

WATU 37 wameripotiwa kuugua na kulazwa kutokana na kuibuka kwa ugonjwa wa kipindupindu katika Kijiji cha Forodhani, Kata ya Korongwe, wilayani Nkasi mkoani Rukwa. Akitoa taarifa kwenye kikao cha dharura cha kamati ya afya ya msingi, Mganga Mkuu wa Wilaya ya Nkasi, Benjamin Chota, alisema taarifa za kuwapo kwa wagonjwa wa kipindupindu ziliripotiwa Desemba 2, mwaka huu na wagonjwa watatu waliripotiwa katika Zahanati ya Korongwe.

Alisema kuwa baada ya taarifa hizo timu ya wataalamu wa afya wilaya kwa kushirikiana na wataalamu wa afya ngazi ya mkoa walielekea katika kijiji hicho na baada ya kuchukua sampuli na kuzipima ilibainika kuwa ni ugonjwa wa kipindupindu na kuchukua hatua za kukabiliana na ugonjwa huo.

Alisema kuwa waliweka kambi kwa ajili ya wagonjwa wa kipindupindu na hadi sasa waliopata matibabu ni 37 na walioruhusiwa kurudi nyumbani ni 25, waliopo wodini wakiendelea na matibabu 12 na hakuna kifo kilichoripotiwa.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Nkasi, Peter lijualikali, aliwataka wataalamu wa afya kuhakikisha wanachukua hatua zaidi ili ugonjwa huo usitoke nje ya kata hiyo na unadhibitiwa uliopoibuka.

Aliwaagiza wataalamu wa afya kuhakikisha wanasimamia suala la usafi katika maeneo yote ya wilaya kwa kuwa kipindupindu ni matokeo ya uchafu na kuwa hatamvumilia mtu ambaye kwa uzembe wake atasababisha ugonjwa huo kusambaa maeneo mengine.

Alisema sheria za kukabiliana na uchafu zipo kinachotakiwa ni kuzitumia ili kuona mazingira ya kuishi yanakua safi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha maji ya kunywa yanachemshwa au kuwekewa dawa.



Waziri wa Usafirishaji na Mawasiliano, Rahma Ali Khamis, akikagua meli ya Ikram ambayo hufanya safari zake Unguja na Pemba waliokaa ni abiria ambao wanaelekea Pemba. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wanafunzi wasimamishwa kujihusisha mapenzi shuleni

**Na Christina Haule,** MOROGORO

BODI ya Shule ya Sekondari Uluguru, mkoani Morogoro, imewasimamisha kuendelea na masomo wanafunzi watatu wa kidato cha tatu kwa tuhuma za kujihusisha na mapenzi shuleni.

Mwenyekiti wa Bodi ya Shule hiyo, Dk. Lusako Mwakiluma, alisema hayo jana kwenye uzinduzi wa matundu 10 ya vyoo vya wasichana vilivyogharimu Sh. milioni 15, alivyovijenga kama zawadi kwa watoto wa kike wa shule hiyo ikiwa ni ahadi aliyojiwekea kama akifikisha shahada ya tatu.

Mkurugenzi Mtendaji huyo ambaye ni wa Taasisi ya Wezesha Mabadiliko (WEMA), alisema walibaini wanafunzi kujihusisha na mapenzi shuleni walipokuwa wakifanya ukaguzi wa vyoo katika shule za halmashauri hiyo.

"Serikali na wadau wa elimu tushirikiane kwa pamoja kukomesha vitendo hivi shuleni kwa sababu watoto wanapaswa kutumia muda wao wote kusoma na kufaulu mitihani yao na sio kujihusisha na uhusiano ambao madhara yake ni makubwa," alionya.

Vile vile, alikumbusha ikiwa wazazi watashirikiana vyema na walimu kuangalia mienendo ya wanafunzi, mimba na ndoa za utotoni vitakwisha kabisa na kubaki na kauli moja kuwa kwa pamoja inawezekana kutokuwa na mimba na ndoa za utotoni.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Uluguru, Festo Kayombo, alisema msaada huo umewaokoa katika adha ya wanafunzi 20 kutumia tundu moja la choo na sasa changamoto iliyobaki ni ya kukosa uzio.

"Uhaba wa vyoo shuleni hapa ulikuwapo kufuatia kuwapo wanafunzi wa kike 360 na matundu ya vyoo 10 ambayo yanakidhi watoto wa kike 200 na kufanya upungufu wa matundu nane, huku wavulana wakiwa na matundu 12 ya vyoo ambayo ni chakavu na kufanya kuwa na upungufu wa matundu ya vyoo matatu," alisema Kayombo. Naye mmoja wa wanafunzi wa kidato cha tatu, Evodi Mkulasi aliomba wazazi na walimu kuwa na tabia ya kufuatilia wanafunzi ili kubaini upungufu wa wanafunzi na kuwaasa wanafunzi wenzie kuacha kujihusisha na mapenzi katika umri mdogo.

Akifungua kikao cha makabidhiano, Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Mwalimu Leah Seleman, alipongeza shule hiyo kwa kuwa ya pili kati ya zilizokuwa na vyoo maalum vya kujisitiria watoto wa kike Manispaa ya Morogoro.

# RC Songwe aitaka TARURA kujieleza

Na Thobias Mwanakatwe

WAKALA wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA), wilayani Ileje, mkoani Songwe 'wamemchefua' Mkuu wa Mkoa huo, Omari Mgumba, baada ya kubadilisha matumizi ya Shilingi bilioni saba zilizotolewa na serikali kwa ajili ya kujenga barabara wilayani humo.

Fedha hizo ambazo zilipitishwa na Bunge ili zitumike kujenga barabara kutoka Kaburo hadi mgodi wa makaa ya mawe Kiwira, TARURA imedaiwa kuzipeleka kwenye mradi mwingine kinyume cha maelekezo ya serikali na bunge.

Kutokana na hali hiyo, Mgumba ametoa siku tatu kwa TARURA Wilaya ya Ileje kutoa maelezo sababu ya kubadilisha matumizi ya fedha hizo.

Alitoa agizo hilo wakati wa ziara yake ya siku moja katika migodi miwili ya makaa ya mawe Kaburo na Kiwira iliyopo wilayani Ileje, mkoani humo.

"TARURA Wilaya ya Ileje nawapa siku tatu mtoe maelezo kwa kina ni kwanini mmeamua kubadili matumizi ya fedha Shilingi bilioni saba zilizotengwa na serikali na kupitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya ujenzi wa barabara inayotoka Kaburo-Mwalisi hadi STAMICO-Kiwira," alihoji.

Aliongeza kuwa, TARURA Wilaya ya Ileje wameiondoa kwenye mpango wa kujenga barabara hiyo na fedha zake kuelekezwa kwenye barabara zingine huku wakitaka ujenzi wa barabara hiyo ufanywe na STAMICO.

Alisema kitendo kilichofanywa na TARURA ni kudharau uamuzi wa serikali na bunge.

Vile vile, alisema bunge lilitenga kiasi hicho cha fedha likitambua umuhimu wa barabara hiyo yenye urefu wa kilometa saba ambayo ingerahisisha usafirishaji wa makaa ya mawe kutoka mgodi wa Kaburo hadi Kiwira penye mtambo wa kuchakata rasilimali hiyo ambao kwa sasa magari hulazimika kuzunguka umbali wa kilomita 38 kupitia wilaya za Kyela na Rungwe.

"Barabara hiyo ni muhimu kwa uchumi wa Ileje, Songwe na taifa kwa ujumla hivyo, itakapokamilika itasaidia kuongeza uzalishaji wa makaa ya mawe pamoja na kuongeza ajira," alisema Mgumba.

Alitaka ujenzi wa barabara hiyo uzingatie mahitaji kwa kuwa magari yenye uzito wa tani 30 yatapita kwa ajili ya kubeba makaa ya mawe.

Akizungumzia kuelekea kilele cha maadhimisho ya miaka 60 ya Uhuru, alisema kuwa mgodi wa Kiwira ni moja ya alama za Baba wa Taifa alizowaachia Watanzania zikionyesha ubunifu katika uongozi na kuendelea na uzalishaji ni sehemu za kuwaenzi waasisi hao.

Samwel Kibarange, Mratibu wa Shughuli za makaa ya mawe Kiwira, alisema ujenzi wa barabara ya kilomita saba utakapokamilika utaongeza kasi ya uzalishaji na kuleta ushindani katika soko la dunia.

Aidha, Kibarange aliiomba serikali ihamasishe wamiliki wa viwanda vya saruji vya ndani na nje kununua makaa ya mawe kutoka STAMICO kwa kuwa uzalishaji wake ni wa kuridhisha na kwa mwaka ujao wanatarajia kuzalisha zaidi ya tani milioni 1.5.

Diwani wa Kata ya Ikinga, kwenye migodi hiyo, Sadock Nyingi, amepongeza juhudi za Mkuu wa Mkoa kwa kutembelea kata yake ambayo imefungua fursa mpya za kiuchumi kwa wananchi.




Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Shaaban, akiwa ameambatana na viongozi na waratibu alipotembelea mabanda ya wajasiriamali katika maonyesho ya 21 ya wajasiriamali wadogo na kati wa Afrika Mashariki maarufu 'Nguvu Kazi au Jua Kali' yanayofanyika Viwanja vya Rock City Mall jijini Mwanza. **PICHA: ADAM HAULE**

# Simiyu yakabiliana uharibifu mazingira

**Na Happy Severine,**
BARIADI

MKOA wa Simiyu ni miongoni mwa mikoa mitano kinara inayoongoza kwa uharibifu wa mazingira kwa ukataji wa miti kikiwa ni kiashiria hatarishi cha kusababisha ukame ndani ya mkoa huo.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Mkoa huo, David Kafulila, wakati wa uzinduzi wa Siku ya Mama Samia iliyozinduliwa mjini Bariadi.

Kafulila alisema tatizo la uharibifu wa mazingira kwa kukata miti ovyo limekuwa kubwa ndani ya mkoa huo, na kwamba mkoa huo umetajwa kuwa moja ya mikoa mitano inayoongoza kwa ukataji miti.

"Bado nchi inakabiliwa na tatizo la ukataji miti...na tatizo hili si kwa Tanzania tu, bali duniani kote na endapo hatutalizingatia, nchi na mkoa wetu vitabaki kuwa jangwa," alisema.

Alizitaka halmashauri zote kuhakikisha zinatimiza lengo la serikali la upandaji miti milioni 1.5 kila mwaka.

Mkuu wa Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu, Lupakisyo Kapange, alisema katika kutambua jitihada na maendeleo yanayofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan, wameamua kupanda miti 5,000 kuunga mkono juhudi hizo.

Ofisa Tarafa ya Ntuzu, Rashid Zongo, akipokea miche ya miti hiyo na kuahidi kusimamia upandaji wake na kutoa taarifa kila wiki.

## Mifumo yaendelea kuboreshwa kuwainua wanasayansi, wabunifu

Na Elizabeth Zaya

SERIKALI imesema itaendelea kuboresha mifumo, sera na sheria kwa ajili ya kuweka mazingira mazuri ya kutengeneza wanasayansi na wabunifu mahiri, wazawa ili wasaidie nchi katika ufumbuzi wa changamoto mbalimbali.

Kauli hiyo ilitolewa jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Dk. Amos Nungu, wakati akifungua hafla iliyoandaliwa na Taasisi ya Wanasayansi Chipukizi (YST) kwa ajili ya kutangaza na kutoa zawadi kwa wanafunzi waliofanya vizuri kwenye miradi mbalimbali ya ubunifu.

Alisema tayari serikali imetambua mchango unaofanywa na YST wa kuibua vipaji vya kisayansi kupitia wanafunzi inayoendesha kila mwaka kwenye shule mbalimbali nchini na kwamba itahakikisha kazi za kibunifu zinazoibuliwa na wanafunzi hao zinawekwa kwenye vitendo kwa kuziboresha zianze kutumia kusaidia jamii.

"Na ndio maana serikali lazima tuendelee kuweka mazingira mazuri, ikiwamo kuboresha mifumo, sera na sheria zitakazotupatia wanasayansi na wabunifu wengi kama hawa wanaozalishwa na YST."

Ofisa Mtendaji wa Taasisi ya Karijmee Jivanjee Foundation(JKF) ambao ni miongoni mwa wadhamini wakubwa wa tuzo hizo za YST, Caren Rowland, alisema wako tayari kuendelea kusaidia kuibua kwa wanasayansi hao kwa sababu ndio ingini ya uchumi kwenye taifa.

"Tumedhamini tuzo hizi miaka yote na tumeona matunda yake, baadhi ya wanafunzi walipitia huku hadi sasa wapo waliopo vyuo vikuu na wengine ni madaktari,"alisema Caren.

Miongoni mwa wanafunzi waliofanya vizuri katika tuzo hizo mwaka huu ni Agnes Kasonso na Vitoria Mnembezi kutoka Shule ya Sekondari Milundikwa iliyopo mkoni Rukwa ambao walishinda kwa kubuni utengenezaji wa taulo za kike zilizosaidia wanafunzi katika shule tano za sekondari mkoani kwao.

Mwenyekiti wa Bosi ya YST, Prof. Yunus Mgaya, alisema jambo linalofanywa na taasisi hiyo ni kubwa sana, na inatekeleza jukumu ambalo litasaidia serikali kwa kiwango kikubwa kuzalisha wanasayansi na wabunifu wazawa hususani katika kipindi hiki cha serikali kujenga uchumi wa viwanda, uchumi wa viwanda.

Mkurugenzi Mtendaji wa YST, Dk. Gozibert Kamugisha, alisema katika jitihada za kuimarisha ujuzi shuleni, taasisi hiyo imekuwa ikitoa mafunzo kwa wanafunzi wa shule za sekondari ikiwa ni maandalizi ya maonyesho ya kisayansi ambayo yalianza tangu mwaka 2011 ambayo mwaka huu yalifanyika kila mkoa.

Alisema mwaka huu jumla ya wanafunzi 2,376 waliwasilisha maombi ya kazi 594, kazi 30 zilipatiwa zawadi za ushindi, na 16 bora zaidi zilichaguliwa kushiriki katika tuzo kitaifa, Dar es Salaam.

Nipashe
# TESA
Jumanne Desemba 14, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI


Ukurasa 14

Awamu sita kufungua mwaka na sekondari mpya za kata 214

Ukurasa 13



## HATARI WASICHANA VVU UMATI, ACTIONAID wanapotaja mbinu za kutumiwa kuwanusuru

ELIMU

NA ELIZABETH ZAYA, ALIYEKUWA MPWAPWA

HATARI MIMBA UTOTONI...

# Ushuhuda binti, nduguze watelekezewa bibi, wasoma kupitia 'umachinga mkaa'

•Mdau elimu: Ninawanusuru kila wanapoelemewa



Wadogo wa Christina katika umachinga wa mkaa, mitaani Mpwapwa. **PICHA: ELIZABETH ZAYA.**

NI saa saba mchana nikiwa kwenye 'bodaboda' katika mizunguko yangu ya kawaida mji wa Mpwapwa, nakatiza katika eneo la Igovu huku jua kali la utosi linawaka, nawaona watoto watatu wamejitwisha mifuko, kichwani huku wakiita 'mkaa...mkaa...'

Bila kusita namwomba mwendesha bodaboda aliyenipakia asimame kwanza, ili nifuatilie na kubaini walichokibeba na wanachokifanya watoto hao.

Nikiwa nimetulia pale ninawaona wanapita kwenye nyumba ya kwanza wanabisha hodi huku wakisema 'tunauza mkaa.' Nikaona anatoka mtu na kuwaambia, 'asante leo hatuchukui.'

Wakatoka kwenye nyumba hiyo na kuingia nyumba iliyofuata, nami nikawa nawafuata kwa nyuma. Hapo napo wakabisha hodi na kusema... 'tunauza mkaa.' Akatoka binti na kusema "...piteni kesho, bado tunao."

Wakati wanatoka kwenye nyumba hiyo ya pili nikiwa nawafuatilia, nikawaita na kuwaomba nizungumze nao. Mmoja ndiye anaonekana anamwongoza mwenzake, akaniambia wako tayari kwa sharti: "Sawa dada ila tunaomba tusichelewe sana, tunawahi wateja tukauze mkaa tumpelekee bibi pesa."

Baada ya kukubaliwa, nilimlipa dereva bodaboda pesa yake ya kunizungusha na akaondoka. Hapo nikatafuta kibanda cha mama lishe na kumwomba atupatie viti na meza tuketi nje, eneo la faragha kulikokuwa na kivuli cha mti.

Kabla ya kuanza mazungumzo, nilimwagiza mama lishe atuhudumie chakula wote watatu chakula, kwani walionekana wamenyong`onyea kwa njaa na uchovu, wakiwa wamechafuka sana kuanzia miguuni hadi kichwani.

Niliwauliza, endapo mtu akitaka kununua mzigo wote wa mkaa waliokuwa wamebeba ilikuwa shilingi ngapi, wakasema Sh.10, 000. Kwa hiyo, nikawapatia ile pesa.

Nilifanya hivyo ili wawe huru kuzungumza nami, hata chakula kilipoletwa, walikula kwa utulivu huku tukiwa tunazungumza ya kawaida kutambulishana na kuzoeana.

Tukiwa tunazungumza na kucheka, mmoja aliyejitambulisha

INAENDELEA UK.12

# Ushuhuda binti, nduguze watelekezewa bibi, wasoma kupitia 'umachinga mkaa'

INATOKA UK.11

kwa jina Christina (sio jina lake halisi) mwenye umri miaka 13, anajitambulisha ndiye dada yao, akisema: "Tumefanya biashara hii kwa muda mrefu, sasa hivi niko darasa la sita, lakini tangu darasa la pili nilikuwa nimeanza kuuza mkaa."

Anasimulia kwa mama yake wamezaliwa wawili, yeye na mdogo wake wanafanya biashara hiyo na wanaishi na bibi yao, pamoja na wajukuu wengine wanne, tangu waachwe hapo na wazazi wao miaka mitano iliyopita.

"Mama yetu sisi wawili alifariki na baba yetu alioa mke mwingine ambaye wanaishi naye Ifaraka. Alituacha kwa bibi ambako tunaishi na watoto wengine wanne na wenyewe wazazi wao waliwaacha hapo, baada ya kutengana, jumla tuko sita na bibi ni wa saba," anaeleza binti huyo.

"Maisha yetu ni magumu sana, kwa sababu tangu tuachwe kwa bibi, baba yetu hatujali na wala wale wengine wazazi wao nao ni kama wamewatelekeza. Bibi peke yake ndiye amekuwa akituhangaikia," anaendelea.

Nipashe ilimfuata Bibi wa Christina, ambaye hakutaja jina lake nyumbani na alikiri ugumu wa maisha kuwalea wajukuu hao, hasa anapokosa pesa za matumizi na hivyo kupitia biashara hiyo, ndiyo imebaki mkombozi kwao.



Christina na nduguze wakiwa katika harakati za kuuza mkaa, mitaani Mpwapwa. **PICHA: ELIZABETH ZAYA.**

### BIASHARA MKAA

Mtoto huyo anaeleza kwamba, baada ya maisha kuzidi kuwa magumu, bibi yao alimpatia mtaji Sh.10,000 ili akanunue mkaa auze.

Anasimulia kwamba alifanikiwa kununua mkaa gunia moja kwa bei ya Sh.9, 000 wakiuza na kutembeza nyumba moja baada ya nyingine na huwa inamchukua siku nne kumaliza gunia, ili kupata fedha Sh.12, 000.

"Shilingi 3,000 ya faida nilimkabidhi bibi yangu na Sh.9, 000 nikanunua tena mkaa, niliendelea kufanya hivyo na pesa ya faida ndio ilikuwa ya matumizi yetu kwa ajili ya kununulia chakula. Kwa sasa ndio nashirikiana na hawa wadogo zangu wawili tunauza pamoja.

"Gunia moja tunauza kwa siku mbili, tunafanya biashara jioni tukisharudi shuleni labda siku ya Jumamosi ndio tunaanza asubuhi na jioni tunawahi kurudi kufua nguo.

"Mimi nikijitwisha debe mbili, wadogo zangu wanajitwisha debe moja moja, wakati mwingine unaisha au unabaki na unaobaki huwa tunaomba tunauhifadhi kwa mtu na kesho yake tunauchukua, lakini, ndani ya siku mbili gunia linaisha lote," anaeleza.

Bibi wa Christina, ambaye hakutaja jina lake pale Nipashe ilipomfuata nyumbani, alikiri ana ugumu wa maisha kuwalea wajukuu hao, hasa anapokosa pesa za matumizi, hivyo kupitia biashara hiyo za wajukuu zake, ndiyo mkombozi wa maisha yao.

### MAOFISA SERIKALI

Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Mpwapwa, Fadhili Mollel, anasema katika wilaya hiyo bado ina matukio mengi ya watoto kutelekezwa na wazazi wao na kutokana na ukubwa wa tatizo, wamekuwa wakizunguka katika kata mbalimbali kutoa elimu kwa wazazi na walezi kuhusu umuhimu wa kutunza watoto.

"Wengi wao hawatoi kipaumbele kwanza kwenye malezi ya watoto wao kwa ujumla na linapofika suala la 'kuwa -support' (kuwaunga mkono) kwenye elimu, inakuwa tatizo jingine, wanaona kama ni kazi ya serikali kuwahudumia kila kitu,"

"Wapo ambao tumekuwa tukiwafikisha kwenye vyombo vya sheria, lakini kesi zinapokaribia mwisho, huwa baadhi ya mashahidi wanakimbia, Kwa hiyo, unakuta tunakosa nguvu na kesi zinaishia katikati," anasema Ofisa Elimu Mollel.

Mdau na mwanaharakati anayejitambulisha 'rafiki wa elimu' wilayani Mpwapwa, Regina Tarimo, anasema wanakutana sana na matukio ya wanafunzi kutelekezwa wilayani humo na uzoefu wao, wanapowafuata kwenye makazi yao, wengi huwa wameachwa kwa bibi zao ambao hawana nguvu za kuwahudumia.

"Kwa hiyo, wakati mwingine inakubidi ubebe mzigo wewe mwenyewe kutafuta namna nyingine ya kuwasaidia, kwa kuwaelimisha wasijiingize kwenye vishawishi vya kimapenzi, kwa sababu wengi wao huwa wanaishia huko," anaeleza.

Mkurugenzi Mtendaji wa asasi isiyo ya kiserikali inayojishughulisha na kutoa msaada kwa wanafunzi wanaokatisha masomo wilayani Mpwapwa(CDF), Arnold Massawe, anasema licha ya jitihada zao za kuwapigania wanafunzi wote wamalize masomo, wanashindwa kuwadhibiti wote.

"Wakati mwingine unakuta wanashindwa kumaliza, ukiwafuatilia wanasema wanakosa muda wa kwenda kwenye mafunzo, wanakwenda kutafuta vibarua vya kuwapatia pesa au wengine wanabaki nyumbani kusaidia wadogo zao," anasema Masawe.

### MHIFADHI MKAA

Udadisi wa mwandishi ulibaini msamaria mwema aliyekuwa anawahifadhi mkaa watoto hao, pia ni Ofisa Elimu Taaluma Msingi wa Mpwapwa, Agnes Mkacha.

Agnes anaiambia Nipashe kuwa anawahifadhia mkaa, pia anajitishwa jukumu la kuwasaidia anachokitaja 'chochote kile' kama chakula na pesa kidogo kuwasaidia mahitaji madogo ya shule.

"Mimi nilikutana na watoto hawa walipokuja kupiga hodi nyumbani kwangu wakiuza mkaa. Sikuwa na jiko la mkaa, lakini niliwaonea huruma, ikabidi niwadadisi sababu za wao kujitwisha mzigo mkubwa namna hiyo katika umri walio nao.

"Baada ya kunielezea kwa kina, nikabaini kwamba wametelekezwa na wazazi wao na hivyo inawabidi kufanya hivyo ili kuendesha maisha.

"Maelezo yao yaliniumiza sana na ilibidi ninunue mkaa wao wote siku ile na kuanzia hapo wakawa wamenizoea na wakaniomba wawe wanakuja kuhifadhi mkaa wao hapa wanaposhindwa kumaliza huko wanakotembeza," anasimulia.

Anafafanua wasiwasi wake kwa Christina, kwamba huenda malengo yake kielimu yasifikiwe, kutokana na kubeba mzigo mzito wa kulea familia kama dada mkubwa, licha ya kuwa na umri mdogo alio nao.

"Kwa sasa amenizoea. Kwa hiyo mara nyingi huwa anakuja hapa nyumbani kunielezea namna anavyolea wadogo zake. Yaani amebeba majukumu kama mtu mzima," anadokezaa Agnes na anaendelea:

"Amekuwa akihakikisha wadogo zake wanakwenda shuleni, wanapata chakula hata kama ni kidogo na wanasaidiana kufanya hiyo biashara kuendesha maisha yao."

"Nilipoona hivyo, ilinibidi nifuatilie shuleni anakosoma maana nilijua lazima atakuwa hafanyi vizuri kutokana na majukumu aliyobeba. Cha kushangaza, nilikuta kwamba amekuwa akishika nafasi ya saba kati ya wanafunzi 60 kwenye darasa lake.

"Wasiwasi wangu ni kwamba bado yuko katika hatari kubwa ya kutokufikisha malengo yake kielimu kutokana na vikwazo anavyokutana navyo kwenye hiyo biashara yake."

Ofisa Elimu huyo, anaeleza kwamba hadi sasa anaendelea na jitihada kumsaidia binti huyo kumwondoa katika hatari ya kukatisha masomo, akishauri haja ya serikali kuangalia namna ya kushughulika na wazazi wanaotelekeza watoto wao.

"Mimi nasimamia elimu msingi kwenye halmashauri yetu ya Mpwapwa na miongoni mwa vitu vinavyochangia watoto wengi kuwa watoro au kupata mimba na kukatisha masomo ni watoto kutelekezwa," anasema Agnes.

Ofisa Elimu Msingi, Agnes, anaeleza picha ya takwimu, wasichana waliosajiliwa kufanya mtihani wa darasa la saba mwaka 2019 walikuwa 3,649 lakini walioingia kwenye mtihani huo walikuwa 3,553, huku 96 wakishindwa kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo utoro.

Anasema mwaka uliofuata 2020, mabinti wa darasa la saba walisajiliwa 3,485 na waliofanya walikuwa ni 3,388, huku 97 wakishindwa kwa sababu kama zilizotangulia.

Mwaka huu, anasema kati ya wanafunzi 3,826 waliosajiliwa, 137 wakishindwa kwa sababu zilezile.

### RIPOTI & SHERIA

Ripoti ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), inabainisha tatizo la wanafunzi kukatisha masomo katika shule za sekondari, lipo zaidi katika madarasa ya chini, hasa kidato cha pili waliokatisha masomo wako asilimia 39.6.

Anataja sababu zake ni utoro unaichukua asilimia 91.6 ukifuatiwa na mimba, asilimia 5.5

Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009, inafafanua wajibu wa serikali, wazazi, walezi na wanajamii kwa ujumla kuwalinda watoto dhidi ya ukatili na ubaguzi dhidi yao.

Kimsingi, kimataifa haki za watoto zinalindwa nyenzo kuu mbili; Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto (CRC) wa mwaka 1989 na Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (ACRWC) wa Mwaka 1990, yote imeridhiwa nchini Tanzania.

Ni hivi karibuni tu, hatua kubwa kitaifa imechukuliwa kugonga mihuri hiyo ya mikataba na kisheria yaliyoridhiwa nchini, Rais Samia Suluhu Hassan, alipotoa fursa kwa wanaokatisha masomo kwa sababu mbalimbali, ikiwamo utoro na mimba, warejee shule lengo ni kutoa fursa watoto waelimike zaidi.

• ***Makala hii inatokana na utafiti maalum aliyoufanya mwandishi wilayani Mpwapwa, wastani wa wiki moja.***

ELIMU
NA MWANDISHI WETU

HATARI WASICHANA VVU

# UMATI, ACTIONAID wanapotaja mbinu za kutumiwa kuwanusuru



Jenister Muhagama Waziri wa Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu, ametangaza kasi ya maambukizi VVU kwa vijana kufikia asilimia 40. **PICHA: MTANDAO.**

**NA MWANDISHI WETU**

DESEMBA 1, Siku ya UKIMWI Duniani mwaka huu unawaacha Watanzania midomo wazi wakihoji ni ipi hatima ya vijana? Ni baada ya serikali kutangaza kuwa maambukizi kwa vijana ni makubwa, asilimia 40 na kati yao wengi ni wasichana.

Wanaoambukizwa ni 'watoto' miaka 15 hadi 24 na asilimia 80 ni wasichana, inamaanisha katika maambukizi 100 themanini ni wasichana, hawa ndiyo wazazi watarajiwa, raia, walipa kodi, wataalamu na wapigakura. Inamaanisha juhudi kubwa za kuwalinda zinahitajika.

Wakati serikali ikitangaza kuwa maambukizi miongoni mwa 'watoto' hao yanatisha na wasichana wanaathirika zaidi, wadau wa elimu ya afya ya uzazi na ujinsia kwa vijana wanakutana Morogoro kutafakari kazi zao na pia mipango ya kuwakwamua vijana na maambukizi ya VVU.

Kuwawezesha kujikinga na mimba za utotoni, ukatili kijinsia na magonjwa ili wasiwe sehemu ya wanaokwamishwa na maradhi na mimba katika umri mdogo na taifa kuwa na wanawake wengi walioathirika na VVU.

Shirika la Kimataifa la ActionAid Tanzania (AATZ) ni miongoni washirika wa kutoa huduma za elimu ya afya ya uzazi na ujinsia kwa vijana likifanyakazi na Chama cha Uzazi na Malezi Bora ( UMATI) katika wilaya za Mbozi mkoani Songwe na Kilosa, Morogoro, anasema Samweli Mkwattwa, kwenye mkutano huo.

Mkwattwa Meneja wa Mradi wa Uimarishaji wa Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii ( (PSA), unaoiamsha jamii kufuatilia, rasilimali za umma, kudai haki na kuwa sehemu ya kupanga vipaumbele kwenye huduma za afya, anasema bila vijana kulindwa na kuepushwa na VVU, taifa haliko salama.

Anasema PSA na ActionAid na UMATI wanatoa elimu ya afya ya uzazi na ujinsia, ili kupunguza na kuondoa UKIMWI kwa vijana, na miongoni mwa changamoto wanazozigundua ni kukosekana vituo bora vya kutosha vinavyotoa huduma za kuwaelimisha vijana afya ya uzazi na ujinsia ili kujitambua. Juhudi zinahitajika kuwafikia vijana zaidi kutokana na changamoto za kukosekana bajeti ya kutosha kutoa elimu hiyo, wataalamu wa kutosha wa kuwapa vijana elimu ya uzazi na ujinsia, anawaambia washiriki.

"Tumegundua kuna ushiriki mdogo wa vijana kwenye masuala ya kijamii, hivyo PSA inatatua kwa kuanzisha majukwaa ya vijana kwenye ngazi za vijijini, kata na wilayani ili wadai na wapate huduma, tena zitolewe ipasavyo na serikali itenge bajeti ya kutosha ili kuondoka na maambukizi hayo baada ya kuwaelimisha vijana..."

**NINI KINACHOFANYIKA?**

Ofisa wa Vijana wa Taifa - UMATI, anayeshiriki mkutano wa wadau wa afya ya uzazi, Upendo Daud, anazungumza na Nipashe, akisema baada ya kugundua mapengo kadhaa yanayochangia kuenea VVU na mimba utotoni, wanatekeleza mradi wa PSA wilayani Mbozi (Songwe) na Kilosa (Morogoro) kwa kushirikiana na ActionAid, kuwafundisha vijana kujitambua na kufanya maamuzi sahihi kwenye uzazi na mambo ya ujinsia linapokuja suala la ngono.

Anasema mafunzo hayo yalioyanza 2016 yamewezeshwa mabinti waliofikiwa kufahamu kuwa ni vijana balehe na athari za kufanya ngono ni kubeba mimba katika umri mdogo, kupoteza maisha wakati wa kujifungua, kuambukizwa VVU na UKIMWI.

Aidha, kubaki kwenye hali duni na umaskini, kutosoma, kukosa msaada wa kutosha wa familia ili kulea watoto na kukimbiwa na wanaume wanaoogopa kifungo cha miaka 30 jela, endapo watapatikana na hatia za kubaka, anasema Upendo.

Anaongeza: "Tumewafundisha kujitambua na kuacha kujamiiana mpaka wakati utakapofika. Kudai huduma za afya ya uzazi salama na ujinsia, kushiriki katika vikao vya kijamii, kupata fursa za mafunzo kama ya ujasiriamali, uongozi, kujua na kufuatilia haki zao mfano mikopo ya vijana, wanawake na wenye ulemavu kwenye halmashauri."

Kwa upande wa vijana wa kiume waliojitambua hawawezi kuwapa mabinti mimba, hivyo kujiepusha na kesi mahakamani, magonjwa, ndoa za kulazimishwa na kuachana na mila potofu zinasababisha wanaume kuendeleza ukatili dhidi ya wasichana, kunyanyasa na kuwanyanyapaa dada zao, anasema Pendo.

"Wanaepuka maambukizi ya VVU, kuingizwa kwenye umaskini, kulea familia bila fedha, elimu wala mali au ujuzi na migogoro ya kisheria hata kifungo," anasema Upendo.

**WANACHOFUNZWA**

"Vijana wanaelezwa kuhusu jinsi ya kutumia njia na mbinu za kujiepusha na mihemko, kuacha makundi rika, mimba na magonjwa ya kujamiiana katika umri mdogo, anasema ofisa wa UMATI.

Anaongeza kuwa mafunzo yanatolewa kulingana na umri wa vijana: "Wapo watoto kuanzia miaka 10 hadi 15 huwezi kuwaambia watumie mipira ya kiume au vidonge. Tunawaambia wasishiriki ngono utotoni na jinsi gani wafanye kuepuka kuiingiza kwenye makundi rika, kujiepusha na vishawishi mbalimbali vinavyowapoteza," anasema Ofisa Vijana wa UMATI.

"Mafunzo yanatofautiana vijana wanaelezwa kuhusu mabadiliko wanayoyapata mwilini, athari mfano mimba, magonjwa, lakini wakubwa zaidi walioanza kujamiiana lazima waambiwe kuhusu kupata mimba, magonjwa, utoaji mimba usio salama, taarifa za uzazi salama na wapi wanapopata huduma hizo iwe vituo vya afya au zahanati."

Upande wa wilaya za Kilosa na Mbozi mwitikio ni mkubwa mafunzo yameunda vikundi vya vijana 15 mpaka 25 katika vijiji vilivyopatia mafunzo na vikundi viko 62, Mbozi vipo 22 na Kilosa vikundi 40 vikiwa na vijana hadi 30 waliojengewa uwezo wa kujua hali zao, athari za ngono, kudai haki za huduma na wapi pa kuzipata pamoja na mbinu za uwekezaji ukiwamo ujasiriamali ambao wamewafikishia ujumbe vijana wengine wengi.

Anataja kuwapo mabadiliko yanayoonekana kwenye maeneo hayo, mfano vijana wanadai na kufuata taarifa za huduma rafiki za uzazi salama na ujinsia. Msukumo huo umeleta kujengwa kituo cha Mvumi wilayani Kilosa kwenye hospitali ya kata na huduma zinatolewa baada ya halmashauri kujenga chumba cha kuhudumia vijana, pia Kijiji cha Itaka wilayani Mbozi kuna chumba na huduma hizo.

Anasema vijana wamekuwa sehemu ya kamati za afya za vijiji na kata suala la uelimishaji na kutahadharisha vijana kuhusu VVU, mimba shuleni na utotoni linafanyika na wengi ni wajumbe wa kamati.

Anataja baadhi ya vikwazo kuwa ni kuwapo 'mashuga dadi' wanaotumia udhaifu wa mabinti na umaskini wa familia kuwahadaa. Aidha, wanafunzi kulazimika kutembea kilometa nyingi kwenda na kurudi nyumbani kila siku.

"Njia wanazopita ni vichaka na mapori na mabinti hao ni lazima wakumbane na shugadadi wanawapa zawadi kama maji ya kunywa, lifti, pesa za chips, vitabu na matokeo yake ni uhusiano kisha mimba," anaonya Upendo.

"Elimu tunayowapa inataja vitu vyote hivyo, hasara na athari za kujiingiza kwenye uhusiano na kupenda zawadi za 'shugadadi hao. Tunawajengea uwezo wa kukataa upendo wa wanaume hao, kukataa vitu vyao, lakini kuwaonya wanafunzi na vijana wanaobalehe kuachana na makundi rika na kuepuka vibandaumiza vinavyoonyesha picha za ngono."

Anaongeza kuwa katika mafunzo vijana wanataja shida zinazowaingiza kwenye uhusiano katika umri mdogo mfano ukosefu wa huduma kama maji, shule kuwa mbali na kukosa mabweni, umeme shuleni na ndani ya jamii.

"Ndiyo maana mradi unawashirikisha viongozi wa serikali na wadau kuwekeza kwenye huduma za kijamii kama maji, mabweni, chakula shuleni kwani zinapokosekana zinaumiza watoto na kuchangia maambukizi ya VVU, mimba utotoni na kuongeza umaskini."

Anasema Rais Samia Suluhu Hassan, anasema anaumizwa na vifo vitokanavyo na uzazi ambavyo ni matokeo ya huduma duni za afya, mimba utotoni, utoaji mimba usio salama, ukatili kijinsia na kukosekana uelewa wa elimu ya uzazi salama.

"Tunaungana na serikali na tutahakikisha tunapunguza mimba za umri mdogo zinazochangia vifo vya uzazi ambavyo ni kilio cha muda mrefu cha wanawake. Tunachoomba ni bajeti iongezwe na uwekezaji kwenye suala la kuboresha huduma za uzazi na elimu ya ujinsia kwa vijana," anasema.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Awamu sita kufungua mwaka na sekondari mpya za kata 214

- Mabinti, Rais awasikia, kawaneemesha
- Mikoa 10 kila moja shule ya wasichana
- Waziri Ummy: Miezi 6 ikamilike, kasoro...



Wanafunzi wa sekondari za kata wilayani Handeni, wakitembea kuelekea shuleni.

NI wikiendi iliyopita nchini kulikuwapo maadhimisho ya Miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara, Sekta ya Elimu ikiwa miongoni mwa maeneo yaliyopata mafanikio makubwa.

Pia ni wiki kadhaa sasa tangu kutajwa majina ya waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka ujao.

Ilibainishwa wakati wa maadhimisho hayo kuwa idadi ya shule za msingi imeongezeka kutoka 3,270 mwaka 1961 hadi 18,546 mwaka huu.

Wanafunzi nao wameongezeka kutoka 486,470 mwaka 1961 hadi kufikia 11,196,788 (milioni 11.197) mwaka huu. Walimu pia wameongezeka kutoka 9,885 mwaka 1961 hadi 197,929 mwaka huu.

Kwenye ngazi ya elimu ya sekondari, shule zimeongezeka kutoka 39 wakati wa uhuru mwaka 1961 hadi kufikia 5,289 mwaka huu, wanafunzi wa sekondari wameongezeka kutoka 11,832 mwaka 1961 hadi kufikia 2,671,927 mwaka huu huku walimu wao nao wakiongezeka kutoka 764 mwaka 1961 hadi kufikia 190,335 mwaka 2021.

Serikali nayo imeendelea kutilia mkazo zaidi uboreshaji elimu ya sekondari nchini, kwa kuimarisha miundombinu ya kujifunza na ufundishaji.

**UWEKEZAJI MPYA**

Mwaka huu Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) tayari imeshapeleka kiasi cha Sh. bilioni 100.58 kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari mpya 214, zitakazojengwa kwenye kata za majimbo yote nchini.

Pia kuna Sh. bilioni 30 zimepèlekwa kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari mpya za wasichana kwenye mikoa 10 (shule moja kila mkoa) Tanzania Bara.

Ni fedha zilizotolewa kupitia Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari nchini (SEQUIP), unaotekelezwa kwenye shule za sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi sita kwa muda wa miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2020/21 hadi 2024/25.

Utekelezaji wa mradi huo, umeelekezwa kwenye maeneo ya vipaumbele vya serikali yanayogusa moja kwa moja elimu ya sekondari, ambayo ni pamoja na ujenzi wa shule mpya za sekondari zipatazo 1,000.

Shule hizo zinajengwa katika kata zisizo na shule za sekondari na maeneo yenye wanafunzi wengi, kulinganisha na miundombinu iliyopo na ujenzi wa shule mpya za sekondari za wasichana za mikoa 26 ambazo katika kila mkoa itajengewa shule moja.

Ujenzi wa shule hizo utakuwa unafanyika kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana na kwa sasa ofisi hiyo inaendelea na uchambuzi ili kujenga shule za nyongeza 20 kwenye kata zenye msongamano wa wanafunzi.

Gharama ya ujenzi wa shule za sekondari za kata ni Sh. milioni 600 kwa kila shule na kiasi kilichopelekwa katika awamu hii ya kwanza ni Sh. milioni 470.

Vilevile, gharama ya ujenzi wa shule za sekondari za wasichana za mikoa ni Sh. bilioni nne ambapo huku kiasi cha Sh. bilioni tatu kimetolewa ikiwa ni malipo ya awamu ya kwanza ya ujenzi kwa kila shule.

Shule za sekondari za kata zitakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi wasiopungua 400 kuanzia kidato cha kwanza hadi nne na shule za wasichana za mikoa zitachukua wanafunzi wasiopungua 1,000 kwa kila shule.

Mradi huo wa SEQUIP umelenga kuongeza fursa ya upatikanaji wa elimu ya sekondari, kuweka mazingira salama ya elimu kwa wasichana na kuhakikisha wanafunzi wote wanapata elimu bora ya sekondari.

**MAELEKEZO YA WAZIRI**

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Ummy Mwalimu, ametoa maelekezo kwa wakuu wa mikoa na wakurugenzi wote wa halmashauri, kuhakikisha maeneo yaliyoteuliwa kwa ajili ya ujenzi wa shule hizo, hayana migogoro ya umiliki wa ardhi.

Vilevile, halmashauri za majiji na manispaa ambazo zina ufinyu wa maeneo ya ujenzi, wanaruhusiwa kutumia ramani za ujenzi wa ghorofa, huku halmashauri husika zinatakiwa kuomba kibali cha kutumia kiasi kilichotengwa na mapato ya ndani kukamilisha ujenzi wa shule husika.

Ni maelekezo yanayoendana na aliyotoa Rais Samia Suluhu Hassan, akitaka maeneo yenye ama ufinyu au migogoro ya ardhi, yaangalie namna ya kupata mbadala wa kujenga maghorofa kuondokana na misuguano hiyo.

Pia kazi za ujenzi zinatakiwa kuanza ndani ya wiki mbili baada ya kupokea fedha na mwongozo wa ujenzi na kukamilika katika kipindi cha miezi sita kwa shule za sekondari za kata na mwaka mmoja kwa shule za sekondari za mikoa.

Waziri Ummy anaelekeza lingine ni kuzingatia taratibu za usimamizi wa mazingira na ushirikishwaji wa jamii husika kabla, wakati wa ujenzi na baada ya ujenzi kukamilika, ili kuepuka athari zinazoweza kujitokeza kama vile ukataji miti ovyo, uchafuzi wa mazingira na unyanyasaji kijinsia.

La tano, waziri anawaagiza viongozi hao kuhakikisha mradi huo unatekelezwa kwa kutumia utaratibu wa mafundi jamii (force account) au makandarasi na kuwa gharama za ujenzi kwa kutumia njia yoyote zisizidi fedha zilizotengwa kwa ajili ya shughuli husika.

Ni mradi unaotekelezwa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ukilenga kuboresha elimu ya sekondari nchini.

Fedha za kutekeleza mradi huo zinatolewa na serikali kupitia mkopo wa takribani Sh. trilioni 1.1 kutoka Benki ya Dunia (WB).



Kazi ya ujenzi wa shule ya sekondari ya kata ikiendelea, kwa kutumia mchango wa nguvu za wananchi, mkoani Mara. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



# Vifaa vya World Vision kutunza data za wagonjwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MRATIBU wa afya ngazi ya jamii kutoka Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mary Kombola, amesema vifaa vya TEHAMA vilivyotolewa na Shirika la World Vision vitasaidia kutunza data za wagonjwa katika vituo vya afya.

Kombola aliyasema hayo akipokea vifaa hivyo kutoka kwa Meneja wa Mradi wa Afya ya Mama na Mtoto, Daud Gambo.

Alisema, awali vituo vya afya vilikuwa vinakabiliwa na changamoto ya uhifadhi data hivi sasa tatizo hilo linakwenda kuisha.

"Tumetoa kompyuta hizo Wilaya ya Chemba na Bahi tunaamini tumetatua tatizo," alisema Kombola.

Alisema lengo lao ni kuisaidia serikali kuhakikisha wanaisapoti sekta ya afya hapa nchini.

Aliishukuru Word Vision kwa kuwapa vifaa hivyo, na kwamba wataweza kutoa taarifa kwa usahihi kutoka kwenye vituo kwenda halmashauri ambapo alisema changamoto kubwa ilikuwa ni takwimu kutoingizwa kwa usahihi.

Meneja wa mradi wa afya ya mama na mtoto, Daudi Gambo, alisema kompyuta hizo zimegaiwa katika wilaya hizo ambapo kila wilaya imepata tatu tatu, huku akieleza kuwa vifaa hivyo zitakwenda kuboresha mfumo mzima wa kutoa taarifa na kukusanyaji taarifa kutoka ngazi ya jamii kupitia wahudumu wa afya.

Alisema baada ya kuona wanakabiliwa na changamoto hizo waliona ni vema kutoa vifaa hivyo katika vituo vya afya ili wote wakifanya kazi wawe na takwimu zinazofanana.

Alisema wamekuwa wakitoa vifaa mbalimbali vya sekta ya afya ili kuisaidia serikali kuboresha sekta hiyo.

Hata hivyo, aliwataka wahudumu kuhakikisha wanafanya kazi hiyo kwa bidii ili kuisaidia jamii.

Alisema huu ni mwanzo wataendelea kushirikiana na serikali kuhakikisha wanafanikisha kuinua sekta ya afya.

Noel Mbanguka, mfuatiliaji na mtathmini wa mradi na anayehusika katika mambo ya TEHAMA, alisema vifaa hivyo walivyovitoa kwa wilaya hizo mbili Bahi na Chemba vina thamani ya jumla ya shilingi milioni 50.4, huku akieleza kuwa katika bajeti yao ya mwaka huu wametenga fedha kwa kununua kompyuta hizo 6 kwa kuanzia na wamejipanga kuongeza zingine 6 ili ziweze kusaidia katika maeneo yao ya mradi.

Naye Mustapha Ngwil, mratibu wa takwimu za mtu wa Wilaya ya Bahi, alisema kumpyuta hizo zitakwenda kusaidia ukusanyaji wa takwimu kwani tulikuwa na ucheleweshwaji wa taarifa.

# Poland yaahidi kuendelea kuwawezesha wenye ualbino

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SERIKALI ya Poland imesema itaendelea kushirikiana na Tanzania kuhakikisha kuwa watu wenye ualbino wanapata fursa za mafunzo ili waweze kujiajiri.

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Adventist Development and Relief Agency (ADRA), Dk. Piotr Nouacki, alibainisha hayo alipokuwa akifungua mafunzo ya ujasiriamali yaliyoandaliwa na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) yaliyofanyika Kizota jijini Dodoma.

Dk. Nouacki alisema Dola 87,000 sawa na Sh. milioni 240 zimetolewa na Polish Aid na ADRA Poland kwa ajili ya kukuza ujuzi na elimu ya ujasiriamali kwa watu wenye ualbino katika mikoa ya Dodoma na Morogoro.

Akifungua mafunzo hayo, alisema kuwa serikali ya Poland itaendelea kushirikiana na Tanzania katika kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata fursa za mafunzo ili waweze kujiajiri na kujiongezea kipato na kutatua kero zinazowakabili.

Aidha, aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kutumia muda wao vizuri ili ujuzi watakaoupata kuleta tija kwa maendeleo yao ukizingatia kuwa Poland na Tanzania zimekuwa na ushirikiano mzuri.

"Ujuzi na elimu mnayopata ikawe na tija kwenye maisha yenu, mkafanyie kazi mafunzo mliyoyapata, tutakuwa pamoja na ninyi ili kuhakikisha mtakachokianzisha kinaleta matokeo," alisema.

Kwa upande wake Kaimu Meneja wa SIDO Mkoa wa Dodoma, Justine Kahemela, alisema mafunzo hayo yatawawezesha kuona ni namna gani wataweza kujisaidia.

"Kuna tafsiri iko mtaani kuwa wenye ualbino hawawezi kufanya lolote, lakini ukweli ni kuwa wanaweza, tunawapa ujuzi kwa vitendo ili wanaporudi mtaani waweze kuwa wajasiriamali," alisema.

Alisema katika Wilaya ya Dodoma wamepanga kuwafikia walengwa 150.

Meneja wa mradi, Aidan Herry, alisema mradi huo wenye thamani ya Sh. milioni 240 ni wa majaribio na unaweza kuongezewa muda.

Alisema utatekelezwa katika mikoa ya Dodoma katika wilaya tano za Dodoma, Chamwino, Kongwa, Mpwapwa na Kondoa na katika mkoa wa Morogoro utatekelezwa katika wilaya mbili.

Alisema katika kutoa mafunzo hayo wamelenga wakufunzi wakuu watakuwa kutoka SIDO.

Ofisa Ustawi wa Jamii Jiji la Dodoma, Edward Rwantungamo, alisema mpango huo ni hatua nzuri katika kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata ujuzi ili waweze kujitegemea.

Alisema halmashauri imekuwa ikitoa mikopo isiyo na riba na miongoni mwa wanufaika wa mikopo hiyo ni watu wenye ulemavu.

Alisema wataendelea kutoa ushirikiano kuhakikisha yale yanayofanywa na wenye ulemavu wa ngozi yanafanikiwa.

Mmoja wa wanufaika wa mafunzo hayo, Vaileth Mushi, alisema mradi huo utawawezesha kujiajiri kwenye ujasiriamali.

"Tulikuwa tukipita kwenye changamoto ya umaskini kutokana na kukosa ujuzi lakini sasa wamejifunza mbinu mbalimbali zitakazowasaidia kujiajiri.



Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Doroth Gwajima (kushoto), akimsikiliza Meneja wa Plan International, Adolf Kaindoa, alipotembelea banda la shirika hilo kwenye uzinduzi wa programu jumuishi ya Taifa ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto iliyofanyika jana jijini Dodoma. **PICHA: INRAHIM JOSEPH**

# Miche 10,000 ya miti kuifanya Dodoma ya kijani

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA.

MKOA wa Dodoma umeandaa miche 10,000 kwa ajili ya kukijanisha maeneo mbalimbali mkoani humo, ukiwamo Mji wa Serikali Mtumba.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, akizungumza jijini hapo, alisema miti hiyo inatakiwa kupandwa msimu huu wa mvua unapoanza katika maeneo mbalimbali ya Jiji.

"Tunaendelea na kampeni ya kuhimiza upandaji miti katika maeneo mbalimbali ya Jiji hili la Dodoma," alisema.

Mkuu wa Mkoa alisema wakazi wa mijini hasa wa Jiji la Dodoma kabla ya mvua wanatakiwa kuandaa mashimo kwa ajili ya kupanda miti maeneo kuzunguka nyumba zao.

"Wakazi wa mijini wanatakiwa kuandaa mashimo kupanda miti wakati wenzao wa vijijini wakiandaa mashamba ya kupanda mazao," alisema.

Wananchi wote wanaomiliki ardhi katika Jiji la Dodoma wanatakiwa kupanda miti ya matunda au ya vivuli kabla ya kuanza ujenzi wa nyumba na hadi wanapokamilisha ujenzi wao miti hiyo inakuwa tayari imekua.

Katika kampeni hiyo ya kupanda miti pia mkuu wa mkoa ameziagiza taasisi mbalimbali zinazojenga au kutoa huduma mbalimbali zinatakiwa kupanda miti katika maeneo yao.

Pia vikundi mbalimbali vya wanawake, vijana na wenye ulemavu wanatakiwa kujikita katika kupanda miti katika maeneo mbalimbali mkoani humo.

Mtaka alisema kampeni hiyo ya kupanda miti inatakiwa kupewa msukumo na viongozi wa halmashauri na wilaya zote za mkoa ili kuhakikisha Dodoma inakuwa ya kijani.





# Mgombea wa CCM atangazwa mshindi udiwani bila kupingwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MSIMAMIZI wa Uchaguzi Jimbo la Mbarali, Missana Kwangura, amemtangaza Furaha Chalamila wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwa Diwani wa Kata ya Ipwani, baada ya kufanyika uchaguzi mdogo juzi.

Kwangura alimtangaza Chalamila kuwa diwani baada ya kupita bila kupingwa kutokana na wagombea wenzake waliochukua fomu za kugombea kujitoa kwenye uchaguzi.

Uchaguzi wa udiwani katika kata hiyo uliofanyika baada ya aliyekuwa diwani wa eneo hilo, Mahamud Mlwale, kufariki dunia Agosti 28, mwaka huu.

"Waliochukua fomu za kugombea walikuwa wanne kutoka vyama vya CCM, CCK, UDP na ACT-Wazalendo na vyama vilivyorejesha vilikuwa 2 ambavyo ni CCM na ACT-Wazalendo na ilipofika Novemba 16, mwaka huu, mgombea wa ACT-Wazalendo alijitoa na alikwenda kuapa mahakamani," alibainisha Kwangura.

Aliongeza kuwa Sheria ya Uchaguzi kifungu cha 45 kifungu kidogo cha 2 kinasema kwamba, endapo mgombea atabaki mmoja katika kata, Msimamizi wa Uchaguzi atakubaliana na hiyo hali na atatoa taarifa kwa Tume ya Taifa Uchaguzi (NEC) pamoja na kumjulisha mgombea kwa barua kuwa amechaguliwa, ila atatakiwa kutangazwa siku ambayo uchaguzi mdogo unafanyika kwa mujibu wa ratiba," alisema.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa hati ya ushindi, Chalamila alishukuru kuchaguliwa kuwa diwani na ameahidi kuwawakilisha vyema wananchi kwenye baraza la madiwani ili kutatua matatizo yanayowakabili wapigakura wake. "Nakishukuru chama changu cha CCM kwa kuniamini, hawakukosea kuniteua, nawaahidi kufanya kazi iliyotukuka kupitia sera na ilani ya CCM kwa kushirikiana na wananchi kushughulikia vikwazo vyote kama vile masuala ya barabara, maji, afya, umeme," alisema Chalamila.

Kwa upande wake Karibu wa CCM Wilaya ya Mbarali, Clemence Mponzi, alisema kuwa amefarijika sana kupata diwani mwingine wa CCM baada ya aliyekuwapo kutangulia mbele za haki, na kwamba anajua kuwa diwani mpya atatekeleza ilani kwa yale mambo yaliyoachwa na mwenzake.

Aliwataka wanachama kufuta makundi na kushirikiana na wenzake waliokuwa kwenye kinyang'anyiro na kwa yale yatakayomtatiza asisite kumtafuta ili washirikiane kuyatatua.

Exaudi Kapalila na Graciana Njwilu, miongoni mwa wananchi waliohudhuria kutangazwa kwa diwani mpya, walisema kuwa wamepata kero nyingi sana tangu diwani wao afariki kwani walikosa mwakilishi kwenye baraza la madiwani sambamba na kukosa mtu wa kumpelekea kero zao ili wazifikishe kwa viongozi wa ngazi za juu.

Vilevile walimwomba Chalamila kuanzia pale alipoishia mtangulizi wake hasa katika masuala ya afya na elimu na wameahidi kumpa ushirikiano.



Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Mbarali mkoani Mbeya, Missana Kwangura (kushoto) akimkabidhi cheti cha ushindi wa uchaguzi Kata ya Ipwani, Furaha Chalamila (kulia) wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) baada ya kuibuka kidedea kwenye uchaguzi mdogo wa udiwani uliofanyika mwishoni mwa wiki. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# 'Kuwapa watoto majina mabaya chachu ya ukatili'

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

WAZAZI na walezi katika Wilaya ya Chunya, wamedaiwa kuchangia ongozeko la vitendo vya ukatili dhidi ya watoto, kutokana na kuwapatia majina yasiyostahili katika jamii.

Hayo yalisemwa juzi na Ofisa Elimu Kata ya Bwawani katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Makongolosi Wilaya ya Chunya, Donard Sawanga, wakati wa mahafali ya tatu ya darasa la awali katika shule ya mchepuo wa Kiingereza ya Hollyland Pre and Primary School inayomilikiwa na Lawena Nsonda.

Sawanga alisema kuwa majina yasiyostahili kwa watoto yamekuwa chanzo cha vitendo vya ubakaji na ulawiti katika jamii, hivyo wazazi na walezi wana wajibu wa kuwa walinzi wa watoto wao ili kuepukana na vitendo hivyo.

"Nawasihi wazazi msipende kukubali watoto wetu waitwe wachumba, baby na majina mengine mabaya. Pia kupokea zawadi kwa watu wasiowafahamu, kwani watu hao hujenga mazoea na baadaye kuwabaka watoto," alisema Sawanga.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Shule ya Hollyland, Lawena Nsonda, alisema maslahi bora kwa walimu na wafanyakazi wote ndiyo mafanikio ya shule hiyo na kiu yake ni kuanzisha pia sekondari ili watoto waendelee shuleni hapo na kuwafanya wawe na matokeo mazuri.

"Mikakati yangu ni kuhakikisha walimu na wafanyakazi wanakuwa vizuri kimaslahi ili waweze kufundisha vizuri watoto hawa... moja ya njia ya kufanya shule ifaulishe vizuri ni pamoja na kuboresha maslahi ya walimu na ndicho ninachofanya mimi, ingawa tuna mpango wa kuanzisha sekondari pia ili watoto watakaomaliza hapa waendelee kusoma hapa hapa," alisema mkurugenzi huyo.

Awali Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Kenya Mahada, alisema shule inafanya vizuri kitaaluma ambapo mtihani wa Mock darasa la nne 2021 Wilaya ya Chunya shule hiyo iliongoza kati ya shule 63 za wilaya.

# Jela miaka mitano kwa kuiba mitungi ya gesi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mbeya imemhukumu kutumikia adhabu ya kifungo cha miaka mitano jela Calvin Mvenile (32), baada ya kukutwa na hatia ya makosa mawili ya kuvunja chumba cha biashara na kuiba mitungi ya gesi.

Hukumu hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Hakimu Mkazi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya, Andrew Scout kwenye kesi hiyo namba 18/2021 ambayo mshtakiwa alidaiwa kutenda kosa Mei 8, mwaka huu katika eneo la Sae alipovunja duka la kuuza vifaa vya ofisi na kuiba mitungi sita ya gesi yenye thamani ya shilingi 300,460, mali ya Ruth Mwakijale.

Hakimu Scout alisema mahakama yake imeridhishwa na ushahidi wa mashahidi wa Jamhuri kupitia mashahidi wake sita akiwamo mlalamikaji ambaye wakati wa usikilizwaji wa kesi hiyo aliitambua mitungi yake ya gesi.

Aidha, alisema kwenye utetezi wake mshtakiwa alikana kuvunja jengo la duka akisema akiwa eneo la Eso alikutana na mtu anayemdai ambapo ulizuka ugomvi kati yao na kujikuta wakikamatwa na kupelekwa polisi kisha kufikishwa mahakamani akituhumiwa kuiba mitungi ya gesi.

Pia mahakama hiyo ilimtia hatiani Calvin Mvenile kwa makosa yote mawili ya kuvunja kinyume cha kifungu namba 296 a (2) na kuiba mali hizo baada ya mahakama kusema kwamba imeridhishwa na ushahidi wa upande wa mashtaka bila kuacha shaka yoyote kwamba mshtakiwa alitenda makosa hayo.

Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Hebel Kihaka, aliiomba mahakama kutoa adhabu kali ili iwe fundisho kwa jamii nzima hasa kwa watu wanaoendekeza vitendo vya uhalifu na tamaa ya kupata mali kwa njia ovu na za mkato.

Kutokana na ushahidi huo, Hakimu Andrew Scout, alimhukumu adhabu ya kutumikia kifungo cha miaka mitano jela kwa kosa la kwanza na kwa kosa la pili kifungo cha miaka mitano na adhabu hizo zitaenda kwa pamoja hivyo kutumikia kifungo cha miaka mitano.



# Wakulima walia kushuka bei ya vanila

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAKULIMA wa vanila kisiwani Pemba wamelalamikia kushuka kwa bei kutoka Sh. milioni moja kwa kilo hadi Sh. 400,000.

Wakizungumza na waandishi wa habari juzi baada ya kongamano la kilimo cha viungo lililofanyika kisiwani Pemba, wakulima hao walisema wanunuzi wa zao hilo wanadai kuwa ugonjwa wa UVIKO-19 umechangia kushuka kwa bei ya zao hilo.

Muhammed Ali Mmanga kutoka Kijiji cha Daya Mtabwe Pemba, alisema kuwa kabla ya ugonjwa wa UVIKO-19 walikuwa wakiuza kilo moja ya vanila Sh. 1,000,000, lakini kwa sasa wanauza Sh. 400,000.

Alisema kuwa bei ya Sh. 400,000 kwa kilo moja ya zao hiyo ni hasara kubwa kwao kutokana na ugumu wa kilimo hicho.

"Mimi binafsi kwa sasa nimeamua kufungia ndani vanila nilizonazo kwa sababu bei ya sasa ni hasara kubwa kwangu," alisema.

Aliiomba serikali kuweka utaratibu wa kulinunua zao hilo ambalo lina thamani kubwa kama inavyonunua zao la karafuu.

Alieleza kuwa endapo serikali itaamua kulinunua zao hilo la vanila na mazao mengine ya viungo, wafanyabiashara wataacha kuwalangua wakulima kwa kuweka bei watakazo wao kwa maslahi yao binafsi.

"Tunapowapelekea wanunuzi wetu kununua vanila wanasema kuwa kutokana na UVIKO-19 bei ya vanila imeshuka duniani sasa sijui kama ni kweli au corona imekuwa kama ni kichaka na kutaka kutukandamiza," alisema.

Baraka Masoud Kasezero kutoka Taasisi ya viungo Tanzania (TASPA'), alisema kuwa ushuru ni mkubwa katika kusafirisha bidhaa za viungo ikiwamo vanila hasa ikizingatiwa kuwa soko kubwa la bidhaa za viungo lipo nje ya nchi hasa Bara la Ulaya.

Akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari Ikulu Zanzibar, Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi alisema kuwa serikali haipangi bei ya mazao bali hutokana na soko la dunia lilivyo.

"Hivi karibuni tulikuwa na wasiwasi kuhusu bei ya karafuu kutokana na corona, lakini tunashukuru soko la dunia halikushuka, hivyo kwa upande wa vanila kama bei imeshuka itabidi tuangalie je, kushuka bei kunasababishwa na soko la dunia au wafanyabiashara wanawaumiza wakulima," alisema.

Alieleza kuwa kuhusu kushuka kwa bei ya zao la vanila serikali yake itafanyia kazi ili kuangalia soko la dunia likoje kuhusu vanila na kama litakuwa limeanguka, hakuna njia lazima kukubaliana na hali hiyo.

Tanzania ina aina 30 ya viungo vinavyotumia kilimo hai ikiwamo vanila, karafuu, pilipili manga, tangawizi, pilipili kichaa, mdalasini, iliki, mchaichai na vingine ambavyo hutumika kwa chakula na dawa.

Kaya 1,050 Tanzania zinatarajiwa kufaidika na mradi wa kilimo hai cha mazao ya biashara ya viungo kupitia mradi wa Agri-Connect unaofadhiliwa na Jumuiya ya Ulaya (EU) ambao unawasaidia wakulima kuwatafutia masoko ya mazao hayo.



Mkulima wa Vanila Muhammed Ali Mmanga akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) walipofika shambani kwake eneo la Daya Mtabwe Pemba. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Mabadiliko sheria zilizopitwa wakati ndani ya miezi sita

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo imesema katika kipindi cha miezi tisa ijayo sheria zote zilizopitwa na wakati ambazo ni kikwazo katika utekelezaji wa majukumu ya waandishi wa habari zitafanyiwa marekebisho haraka.

Hayo yalielezwa jana na Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Khamis Abdalla Said, alipokutana na kamati ya wadau wa mapendekezo ya sheria ya habari jijini Zanzibar.

Alizitaja miongoni mwa sheria ambazo zitafanyiwa kazi ni pamoja na mapendekezo ya sheria ya vyombo vya habari ambayo imewasilishwa na wadau serikalini.

Alisema kuwa Rais wa Zanzibar ametoa maagizo kwa watendaji serikalini kuhakikisha sheria zote zilizopitwa na wakati ambazo zinahitaji kufanyiwa marekebisho ziwasilishwe katika vyombo husika kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

Alisema sheria ambazo zimepitwa na wakati haziwezi kuleta mabadiliko yanayotakiwa na wananchi kwa ajili ya kuleta maendeleo na taifa kupiga hatua kubwa ya uchumi.

Alisema wizara imepokea mapendekezo yanatokana na maoni ya wadau wa sekta hiyo, ambayo lengo lake kupata sheria mpya ya habari ya mwaka 2021 itakayokwenda na mabadiliko ya sayansi na teknolojia na kutoa uhuru zaidi kwa waandishi wa habari kufanya kazi sambamba na serikali katika kuleta maendeleo.

Alisema mapendekezo hayo ni sheria ya kufuta usajili wa magazeti, wakala wa habari na vitabu namba 15 ya mwaka 1988 na marekebisho yake namba 8 ya mwaka 1997 na kutunga sheria ya huduma za habari na mambo yanayohusiana na hayo ya mwaka 2021.

Aidha, alisema Sheria ya Magazeti ya Vyombo vya Habari ya Mwaka 1988 ni ya muda mrefu, yakiwamo mabadiliko mengi ya sayansi na teknolojia ya mawasiliano ya habari na elektroniki. Alieleza kuwa kwa mujibu wa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2050 inasisitiza kuwapo kwa matumizi ya sahihi ya teknolojia ya habari ambayo yatasaidia kuleta mabadiliko makubwa ikiwamo kuzalisha ajira kwa vijana.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Umma katika Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA), Imane Duwe, alisema mahitaji ya sheria zitakazokwenda na wakati na mabadiliko ya sayansi na teknolojia kwa waandishi wa habari ni muhimu hatua ambayo waandishi wa habari watakuwa daraja kwa wananchi na serikali.

# Rais Mwinyi: Serikali kuiimarisha Zimamoto

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali ina azma ya kukiimarisha Kikosi cha Zimamoto ili kukabiliana na athari kubwa zinazotokana na matukio ya moto katika hoteli za kitalii.

Dk. Mwinyi allisema hayo juzi katika hafla ya uzinduzi wa hoteli ya kitalii ya Tui Blue Bahari Zanzibar Pwani Mchangani, Mkoa wa Kaskazini Unguja, baada ya hoteli hiyo kuungua moto Januari 16, mwaka huu na kufanyiwa ukarabati mkubwa na kuanza kutoa huduma. Alisema kumekuwa na matukio mengi ya moto ya kuungua hoteli za kitalii, hivyo serikali inajipanga kukiimarisha kikosi cha Zimamoto ili kukabiliana na hali hiyo ambayo imekuwa ikileta athari kubwa katika sekta ya utalii.

Alisema serikali ina kila sababu ya kuunga mkono sekta ya utalii kwa kuzingatia kuwa hiyo ndio sekta mama ya kiuchumi.

Alieleza kuwa uwekezaji katika sekta ya utalii una mambo matatu yanayolinufaisha Taifa, ikiwamo ajira, wananchi kupata soko la kuuzia bidhaa zao pamoja na serikali kupata fedha zitokanazo na kodi, hivyo alibainisha azma ya serikali ya kuimarisha mazingira ya uwekezaji nchini.

Rais Dk. Mwinyi alisema serikali imechukua hatua mbalimbali katika kuimarisha sekta hiyo ili kuvutia watalii, na ndio maana ikaingia mkataba na kampuni ya ADNATA ya Dubai ili kuimarisha shughuli ya utoaji wa huduma katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume pamoja na kuunda kikosi cha utalii ili kuwahakikisha watalii usalama wao wanapofika nchini.

Alisema wawekezaji katika sekta ya utalii wamekuwa wakitoa huduma mbalimbali za kijamii kwa wananchi, ikiwamo afya, elimu na maji hivyo akazitaka mamlaka zinazohusiana na utalii kusimamia jambo hilo ili kuhakikisha wananchi wa maeneo ya uwekezaji wananufaika ipasavyo.

Naye Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Lela Mohamed Mussa, alisema kurejea kwa huduma katika hoteli hiyo kunatokana na juhudi za mwekezaji wake kujitoa na kufanya kazi usiku na mchana na hatimaye kufanikiwa kurejesha huduma hizo ndani ya kipindi kifupi na kwa kiwango bora zaidi.

Alisema kurejea kwa huduma hizo kutaimarisha sekta ya utalii kwa kutoa ajira kwa vijana sambamba na kuchangia kikamilifu pato la Taifa.

Mkuu wa Mkoa Kaskazini Unguja, Ayoub Moahmed Mahamoud, alisema miongoni mwa mafanikio ya mkoa huo katika kukuza uwekezaji, ni pamoja na kumaliza migogoro mbalimbali, ikiwamo wa Hoteli ya Palolo na kubainisha uhusiano mzuri uliopo kati ya mkoa na wawekezaji umekuwa chachu ya mafanikio hayo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), Sharif Ali Sharif, alisema hoteli imefunguliwa baada ya kukamilika kwa matengenezo makubwa baada ya kuungua moto na kusababisha uharibifu mkubwa wa samani na baadhi ya majengo. Alisema kiasi cha Dola 700,000 zimetumika kwa ajili ya uwekaji wa vifaa vya kisasa vya usalama wa hoteli ili kujikinga na majanga. Meneja wa hoteli hiyo, Eric Freinut, aliipongeza Wizara ya Mambo ya Kale na Utalii kwa kuunga mkono kikamilifu juhudi za kuifanyia matengenezo makubwa hoteli hiyo hadi kurejea katika hali yake ya kawaida.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA INAUZWA.


NYUMBA YA GOROFA INAUZWA IPO UKONGA,INAFREM NANE ZOTE ZINA WAPANGAJI,INAFAA KWA MAKAZI AU BIASHARA,BEI MAELEWANO(WAWEZA LIPA KWA **AWAMU) SIMU.0715 244754**

## NYUMBA INAUZWA.

NYUMBA INAUZWA MOROGORO MJINI MASIKA MIL. 100. NI NZURI KWA BIASHARA, INA VYUMBA KUMI NA NNE. KWA MAWASILIANO PIGA SIMU NAMBA: **0745 222 312 / 0715 768 8**

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**ELIA MESHACK MKELA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1330-0052** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya **PRESBYTERIAN** mwaka 2014, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **KBA/RB/84413/2017**

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**FLEXON EPHRAIM LAUWO** Anatangaza kupotelewa kwa kadi za gari zenye namba za usajili **T111 AQC(NISSAN PATROL)/T618 BCR(TOYOTA HIACE)/T630 ALA(TOYOTA CORONA)/T545 BTM(IPSUM)/T745 ALF(NISSAN PICKUP)/T898 BCF(CANTER).** Zimeungua na moto baada ya nyumba kuungua na moto, namba ya sim **0756590628.**
**MOR /MOR/RB/552832/2021**

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**
**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI NA. 45 YA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU CASTO VICENT JOSEPH**
**JACKLINE VICENT MWENDA…………………MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 14 mwezi wa Februari, 2022.

Imesainiwa Dar es salaam, leo tarehe 30 mwezi wa Novemba, 2021.

HIGH COURT OF TANZANIA

NAIBU MSAJILI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Matika Mahakama ya Mwanzo Kihonda Wilaya ya Morogoro**
**Mkoa Wa Morogoro**
**Usimamizi wa Mirathi……08..2021**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MOHAMED HAKI CHITOTO WA LUKOBE**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ASHA OMARY SAID.**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 20/12/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

**Imetolewa Tarehe 13/12/2021**

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA MOROGORO

## TKUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**DEODATUS MICHAEL CHONYA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA **IST** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 662 DFM** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI **KAH/RB/TR/ 614 /2021**

---

**IN THE DISRTICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**MATRIMONIAL CAUSE NO.68 OF 2021**
**THERESIA PAUL LEONARD**
**VERSUS**
**ISAYA ENOCK**

**NOTICE OF DATE OF MENTION/HEARING**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention/hearing on 22nd day of December 2021 at 10:00 am before Hon.**MSAFIRI-SRM**

Your required to appear in this court without failure and you must produce to that day all the documents upon which you intend to reply in support of your case GIVEN under my hand and seal of the court this 2nd day of desember,2021

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**HATI YA KIAPO**

Mimi **MOHAMED SALIM** mwanamume muislam wa slp tanga mkazi wa jiji la Tanga na raia wa jamhuri ya mungano wa Tanzania ninaapa kama ifuatavyo,

1 kwamba jina langu kamili ni **MOHAMED SALIM**
2. kwamba mimi ni mmilikihalali wa kiwanja na 182/1 kitalu B' mnyanjani-jiji la tanga
3. kwamba hati (offer)halisi ya kiwanja hicho
4. kwamba nimeitafuta na hakuna uwezekano wa kuipata tena hivyo naiomba idara ya ardhi inipatie hati nyingine kwa jina la **MOHAMED SALIM** ili niweze kulipia ada za serikali

Nathibitisha kwamba yote niliyotamka hapo juu ni kweli kweli tupu

Sahihi ya Mwapaji ……………

Imethibitishwa hapa Tanga
Leo tarehe 13/12/2021
Mbele ya MUSTAFA MLAWA
Cheo ADVOCATE
Sahihi ……………
Anwani BOX 5412, TANGA

MUSTAFA RAJABU MLAWA ADVOCATE P.O Box 5412 TANGA NOTARY PUBLIC & COMMISSIONER FOR OATHS

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 59 OF 2021**
**In the Matter of the Estate of the Late Daniel Peter Dotto**

**By 1. Sara Joseph Kunambi**
**2. ……………………………………………….**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the **22 day of 12.2021**

Dated at Morogoro this 23 day of Nov.2021.

MAHAKAMA YA WILAYA MOROGORO

RESIDENT MAGISTRATE

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE INCHARGE DISTRICT COURT P.O. Box 660, Morogoro

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Ramaphosa akutwa na Covid-19 wiki chache akikikana kirusi Omicron

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

RAIS wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa amepimwa na kukutwa na ugonjwa wa Covid-19 na anatibiwa kwa dalili zisizo kali.

Ramaphosa alianza kujisikia vibaya siku ya Jumapili, baada ya kuondoka katika ibada ya kumbukumbu ya rais wa mwisho wa enzi za ubaguzi wa rangi wa Afrika Kusini, FW De Klerk mjini Cape Town, kwa mujibu wa taarifa kutoka kwa ofisi ya rais.

Watu ambao waliungana na rais siku hiyo wameshauriwa kutazama dalili au kupimwa.

Rais amepewa chanjo kamili na amekabidhi majukumu yake yote kwa Naibu Rais David Mabuza.

Rais Ramaphosa alirejea Jumatano iliyopita kutoka katika ziara ya nchi za Afrika Magharibi za Nigeria, Ivory Coast, Ghana na Senegal.

Rais alisema yeye na ujumbe wake walipimwa Covid-19, katika nchi zote walizotembelea. Taarifa hiyo ilisema rais alikuwa amepatikana bila virusi hivyo aliporejea.

Kirusi cha Omicron, kinachoambukiza sana, ambacho kimezua wasiwasi wa kimataifa, kilitambuliwa kwa mara ya kwanza nchini Afrika Kusini mwezi uliopita.

Novemba 29, mwaka huu, rais huyo, alilaani marufuku ya kusafiri iliyowekwa dhidi ya nchi yake na majirani zake kutokana na aina mpya ya kirusi cha Corona Omicron.

Rais Ramaphosa alisema amesikitishwa sana na hatua hiyo, ambayo aliitaja kuwa isiyo na msingi na kutaka marufuku hiyo kuondolewa haraka.

Uingereza, EU na Marekani ni miongoni mwa walioweka marufuku ya kusafiri.

Omicron, imeainishwa kama aina ya kuhofisha. Ushahidi wa mapema unaonyesha kuwa ina hatari kubwa ya kuambukizwa tena.

Kirusi hicho kinachobadilika kwa haraka sana, kiligunduliwa nchini Afrika Kusini mapema mwezi huu na kisha kuripotiwa kwa Shirika la Afya Duniani (WHO).

WHO ilionya dhidi ya nchi zinazoweka vikwazo vya kusafiri kwa haraka, ikisema wanapaswa kuzingatia mbinu ya hatari na ya kisayansi.

Walakini, marufuku nyingi zilianzishwa katika siku za hivi karibuni huku kukiwa na wasiwasi juu ya Omicron.

Mkurugenzi wa Afrika wa WHO, Matshidiso Moeti alisema Jumapili: "Pamoja na aina hiyo ya Omicron sasa iliyogunduliwa katika maeneo kadhaa ya dunia, kuweka marufuku ya kusafiri ambayo inalenga Afrika inaathiri mshikamano wa kimataifa."

Rais Ramaphosa alisema hakuna msingi wa kisayansi wa marufuku ya kusafiri na kwamba eneo la kusini mwa Afrika ndilo lililoathiriwa na ubaguzi usio wa haki.

Pia alidai kuwa marufuku hizo hazitakuwa na ufanisi katika kuzuia kuenea kwa aina hiyo hiyo.

"Kitu pekee ambacho katazo la kusafiri litafanya ni kuharibu zaidi uchumi wa nchi zilizoathirika na kudhoofisha uwezo wao wa kukabiliana na janga hili," alisema.

Alitoa wito kwa nchi zilizoweka marufuku kubadilisha maamuzi yao haraka, kabla ya uharibifu wowote kufanywa na uchumi wetu.

Rais Ramaphosa alielezea kuibuka kwa aina ya kirusi cha Omicron kama wito wa kuamsha dunia kuhusu kukosekana kwa usawa wa chanjo, akionya kwamba hadi kila mtu apewe chanjo, aina nyingine zaidi haziwezi kuepukika.

**BBC**

## Marekani yahofia ukatili unaofanywa na waasi Tigray

**New York,** MAREKANI

MAREKANI imesema ina wasiwasi kuhusu madai ya ukatili uliofanywa na vikosi vya Tigray katika maeneo ya Amhara na Afar nchini Ethiopia, msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje, Ned Price amesema.

Idara hiyo, imewataka wahusika wote wenye silaha kuacha kutumia dhuluma dhidi ya raia na kuzitaka mamlaka kuchunguza tuhuma hizo.

Wiki iliyopita, Human Rights Watch (HRW), ilisema vikosi vya Tigray kwa ufupi viliwanyonga makumi ya raia katika kinachoonekana wazi kuwa uhalifu wa kivita katika miji miwili, iliyokuwa chini ya udhibiti wao katika eneo la Amhara.

Mashahidi walieleza wachunguzi wa HRW, kwamba waliona wapiganaji wa Tigray katika vijiji vya Chenna na Kobo, wakiwaua jumla ya raia 49 katika matukio tofauti.

Mauaji hayo, yalitokea kati ya Agosti 31 na Septemba 9, mwaka huu, shirika la kutetea haki za binadamu lilisema.

Limetoa wito kwa Umoja wa Mataifa (UN), kuanzisha uchunguzi wa kimataifa kuhusu uhalifu wa kivita na kuchunguza dhuluma zinazofanywa na pande zote katika mzozo huo.

Marekani pia imetoa wito wa kusitishwa kwa uhasama na mazungumzo kuanza bila masharti yoyote.

Mzozo huo ulianza tarehe Novemba 4, mwaka, wakati serikali ya Ethiopia ilipoanzisha mashambulizi ya kukiondoa Chama cha Tigray People's Liberation Front (TPLF), baada ya wapiganaji wake kuteka kambi za kijeshi za shirikisho huko Tigray.

**BBC**



Waziri Mkuu wa Israel, Naftali Bennett, akiwa na mwenyeji wake, Waziri wa Mambo ya Kigeni wa Umoja wa Falme za Kiarabu, Abdullah bin Zayed Al-Nahyan, alipowasili katika Umoja wa Falme za Kiarabu. Ni ziara ya kwanza ya kiongozi wa taifa la Israel, kwenye nchi hiyo, ambayo ni miongoni mwa mataifa ya Kiarabu yaliyorejesha uhusiano wao rasmi na Israel. **PICHA: DW**

## Kenya yatoa onyo kidiplomasia kwa Ethiopia

**Nairobi,** KENYA

TAARIFA kwenda balozi za kigeni na ofisi za mashirika za kimataifa zilizoko Nairobi. Wizara ya Mambo ya Nje ilisema, itaruhusu upitishaji wowote wa wafanyakazi au vifaa kutoka nchi ya tatu kupitia, Kenya, kama tu wanakidhi vigezo pamoja na idhini za awali.

Kenya inasema, itazuia harakati zozote za upelekaji jeshi au kidiplomasia kupitia eneo lake, baada ya kuhamishwa kwa muda kwa wafanyakazi wa kigeni kutoka Ethiopia kwa sababu za usalama kulingana na gazeti la Daily Nation.

Katika taarifa kwa balozi hizo, ilisema itaruhusu upitishaji wowote wa wafanyakazi au vifaa kutoka nchi ya tatu kupitia Kenya, kama tu wanakidhi vigezo pamoja na idhini za awali.

Maelezo hayo yanayojulikana kama maelezo ya maneno katika misingi ya kidiplomasia hayataji Ethiopia kwa jina, ingawa inasema matukio ya hivi karibuni katika eneo hilo yanaweza kuzilazimisha baadhi ya nchi za kigeni kuhamishia jeshi na wafanyakazi wa kidiplomasia, kwenda Kenya na lazima itifaki ifuatwe katika kufanya hivyo.

**VOA**

# RAIS TFF SHUHUDA FAINALI KOMBE LA TADAYO 2021

**Na Mary Mosha,** MWANGA

MICHUANO ya Tadayo Cup 2021 iliyokuwa ikishirikisha timu 16 za Wilaya ya Mwanga chini ya uratibu wa Mbunge wa Jimbo hilo, Joseph Tadayo, yamehitimishwa juzi katika Uwanja wa CD Msuya kwa Wakongwe FC kutwaa ubingwa baada ya kuibuka na ushindi wa penalti 4-3 dhidi ya Mgagao FC kwenye mechi ya fainali.

**Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa CD Msuya, dakika 90 za mchezo huo zilishuhudi wa zikimalizika kwa sare ya mabao 2-2 ndipo changamoto ya mikwaju ya penalti ilipochukua nafasi yake na Wakongwe FC kuibuka kidedea.**

Kwa kutwaa ubingwa huo, mbali na kombe, Wakongwe FC wamezawadiwa kitita cha Sh. 500,000 huku Mgagao wakiambulia Sh. 300,000 kwa kushika nafasi ya pili wakati Jouma FC wenyewe waliondoka na Sh. 200,000 baada ya kumaliza katika nafasi ya tatu.

Akizungumza wakati wa kutoa zawadi kwa washindi, Mgeni Rasmi katika fainali hiyo, Rais wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Wallace Karia, alieleza kufurahishwa na namna ambavyo wadau wa mchezo husussan viongozi wa wananchi wanavyopambana kunyanyua vipaji vya vijana.

Alisema kutokana na jitihada hizo, TFF kwa kushirikiana na vyama vya mpira vya mkoa, watashirikiana katika kuhakikisha wanamaliza matatizo kwenye sekta ya soka nchini.

"Nimeona mshikamano mkubwa wa ajabu kutoka kwa viongozi wa wananchi, wanachama, kamati ya ulinzi na usalama katika kunyanyua sekta ya mchezo huu hapa wilayani Mwanga, ikiwa wataendelea hivi, tutaona maajabu makubwa kabisa katika sekta hii.

"Viongozi kama hawa ni hazina, kwa kuwa wananyanyua vipaji kwa vijana, nitoe wito kwa vijana wote kutumia fursa hii katika kuleta mabadiliko na kujiongezea kipato, shirikisho tutahakikisha viwanja vinakuwa katika hali nzuri pamoja na kupatikana kwa walimu watakaosaidia kufundisha mpira wa miguu kwa vijana," alisema Karia.

Kwa upande wa mratibu wa michuano hiyo, Mbunge wa Mwanga, Tadayo, alisema lengo mojawapo la mashindano hayo mbali na kuibua vipaji, lilikuwa ni njia mojawapo ya kuifungua Mwanga kiuchumi kupitia michezo huku pia akieleza ujio wa Rais wa TFF kutafungua fursa kubwa kimichezo wilayani hapa.

"Ujio wa Rais wa TFF katika mashindano haya hapa Mwanga kutafungua fursa za kimichezo, kujenga mahusiano ya kiutendaji katika nyanja za kimiundombinu, semina na kozi za walimu, waamuzi na viongozi ambazo zitasaidia kupata wabobezi katika soka," alisema Tadayo.



Rais wa TFF, Wallace Karia, akimkabidhi kombe nahodha wa Wakongwe FC, Bakari Shabani 'Taito', baada ya timu yake kuibuka mshindi dhidi ya Mgagao FC kwa mikwaju ya penalti 4-3 kwenye mechi ya fainali ya michuano ya Tadayo Cup 2021 iliyopigwa katika Uwanja wa CD Msuya, Mwanga mkoani Kilimanjaro. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Abdallah Mwaipaya na anayefuata baada ya Karia, kushoto ni Mbunge wa Jimbo la Mwanga, Joseph Tadayo na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro, Patrick Boisafi (aliyevaa shati ya kijani). **PICHA: MARY MOSHA**

## Riadha Samia Taifa Cup kurindima leo

**Na Saada Akida**

MKURUGENZI wa Idara ya Maendeleo ya Michezo Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Yusuph Singo, amesema leo, mchezo wa riadha utaanza rasmi katika michuano ya Samia Taifa Cup, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Singo alisema mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani, wamethibitisha kushiriki mchezo huo wa mbio fupi.

Alisema mchezo huo utakuwa wa tatu katika michuano ya Samia Taifa Cup baada ya soka na netiboli kufikia hatua ya nusu fainali ambayo itaanza kucheza leo.

"Kwa muda mrefu, hii ni mara ya kwanza tumeona mikoa mingi imekubali kushiriki mashindano haya ya riadha kwa mbio fupi na kati," alisema Singo.

Singo (pichani) alisema tayari katika michezo ya soka na Netiboli imefika hatua ya nusu fainali na timu ya Wanawake Dar Es Salaam imekuwa ya kwanza kukata tiketi ya nusu fainali baada ya kuichapa mabao 2-1 timu ya Mjini Magharibi katika mchezo uliochezwa jana.

Wakati upande wa wanaume Mara na Mjini Magharibi ndizo zilizotinga nusu fainali.

Mara uliipata nafasi hiyo baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Manyara, wakati Mjini Magharibi iliichapa Kusini Unguja 3-0.



# Ndemla ang'aa, Mtibwa Sugar 'ikiiua' Manungu

**Na Adam Fungamwango**

MCHEZAJI wa Simba anayechezea kwa mkopo kwenye klabu ya Mtibwa Sugar, Said Ndemla, amefunga bao la pili na kuipa ushindi wa mabao 2-0 timu yake kwa mara ya kwanza juzi, tangu kuanza kwa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya timu ngumu ya Biashara United.

Alikuwa ni Nzigamasabo Styve aliyefunga bao la kwanza kwa mkwaju wa penalti, Ndemla akishindilia la pili na kuifanya Mtibwa Sugar kushinda mechi yake ya kwanza na ikicheza kwenye uwanja wake wa nyumbani, Manungu Complex, kwa mara ya kwanza msimu huu, baada ya kutokuwapo hapo kwa misimu miwili kutokana na kutokidhi kanuni za kutumika.

Mtibwa Sugar ilicheza mechi saba mfululizo bila kufunga mechi yoyote hadi ilipofika raundi ya nane na kurejea kwenye uwanja wake halisi, ambapo kabla ilitumia viwanja mbalimbali kama CCM Gairo, Jamhuri Morogoro, Uhuru, Dar es Salaam, Mabatini mkoani Pwani na vinginevyo.

Ndemla ambaye ni zao la kikosi cha pili cha Simba, alitolewa mwanzoni mwa msimu huu kwa mkopo kwenda Mtibwa, ikiwa ni mara yake ya kwanza kucheza soka nje ya klabu yake mama na linakuwa ni bao lake la kwanza msimu huu.

Kwa ushindi huo, Mtibwa imechupa nafasi moja, kutoka kuburuza mkia, hadi kwenye nafasi ya 15 ya msimamo wa ligi, ikifikisha pointi tano, iliiacha nyuma Geita Gold ambayo sasa imechukua zamu ya kubeba timu zote ikiwa na pointi hizo hizo tano, lakini Mtibwa ina tofauti nzuri ya mabao ya kufunga na kufungwa.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### BARCA KUSAJILI NYOTA

BARCELONA wanapanga kumnunua winga wa Chelsea na Marekani, Christian Pulisic mwenye umri wa miaka 23, mlinzi wa Ujerumani, Antonio Rudiger mwenye miaka 28 na beki wa pembeni wa Hispania, Cesar Azpilicueta, 32. ***(Mundo Deportivo)***

### DIAZ ATAKIWA LEEDS

LEEDS United bado wana nia ya kumsajili mshambuliaji wa Chile, Ben Brereton Diaz mwenye umri wa miaka 22, licha ya Blackburn kuweka bei ya pauni milioni 25 ili kumnasa. ***(Sun)***

### PHILLIPS AWINDWA WEST HAM

WEST Ham wanamlenga mlinzi wa England, Nat Phillips mwenye umri wa miaka 24, kama mbadala wa Muitaliano aliyejeruhiwa Angelo Ogbonna mwenye umri wa miaka 33, lakini Liverpool wanadai pauni milioni 10 ili kumwachia. ***(Sun)***

### DEMBELE KUMBADILI COMAN

WINGA wa Bayern Munich, Mfaransa Kingsley Coman mwenye umri wa miaka 25, anasitasita kusaini mkataba mpya hapo kwenye uwanja wa Allianz Arena, na ikiwa hatafanya hivyo, mchezaji mwenzake wa kimataifa, Ousmane Dembele, 24, ambaye anakaribia mwishoni mwa mkataba wake Barcelona, ana uwezekano mkubwa wa kuwa mbadala.***(Christian Falk)***

### RODRYGO YUPO SANA MADRID

REAL Madrid hawana mpango wa kumuuza mshambuliaji wa Brazil, Rodrygo mwenye umri wa miaka 20, licha ya kuhusishwa na Liverpool. ***(Fabrizio Romano)***

### LLORIS KUPEWA MKATABA

KLABU ya Tottenham Hotspur imeanza mazungumzo ya mkataba mpya na golikipa wa Ufaransa na nahodha wa klabu hiyo, Hugo Lloris mwenye umri wa miaka 34, kabla ya mkataba wake wa sasa kukamilika msimu ujao wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

### ORIGI AWANIWA MILAN

MSHAMBULIAJI wa Liverpool na Ubelgiji, Divock Origi mwenye umri wa miaka 26, analengwa na klabu ya AC Milan - ambayo inatafuta wachezaji walio tayari kuchukua nafasi ya Zlatan Ibrahimovica. ***(Tutto Mercato)***

### DANJUMA AMULIKWA LYON

LYON wanataka kumsajili winga wa Villarreal, Mholanzi Arnaut Danjuma mwenye umri wa miaka 24. Manchester United na Barcelona pia wanaaminika kufuatilia maendeleo yake. ***(TodoFichajes)***

### COOK ATAJWA NEWCASTLE

NEWCASTLE wataelekeza mawazo yao kwa mlinzi wa Bournemouth, Steve Cook mwenye umri wa miaka 30, baada ya kupunguzwa bei ya kumnunua beki wa kati wa Burnley, James Tarkowski mwenye miaka 29. ***(Sun)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE MCHEZAJI KIJANA ZAIDI KUFUNGA MABAO 100

●●● Katika umri wake wa miaka 22 na siku 357, anakuwa mchezaji kinda zaidi kufikia...

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe amekuwa mchezaji kijana zaidi kwenye historia ya Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, kufunga mabao 100 kwa timu moja kwa bao lake la pili katika mchezo wa Paris Saint-Germain dhidi ya Monaco, Jumapili.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa alianza kufunga bao la uongozi kwa mkwaju wa penalti dakika ya 12 dhidi ya klabu yake hiyo ya zamani pale Parc des Princes baada ya Djibril Sidibe kumfanyia faulo, Angel Di Maria eneo la hatari.

**Krosi ya Youssouf Fofana ikanaswa na Lionel Messi na mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Argentina akammegea pande Mbappe, ambaye alifunga na kufikisha bao lake la 100.**

Katika umri wake wa miaka 22 na siku 357, Mbappe ni mchezaji kijana zaidi kufikia mafanikio hayo kwa klabu moja kwenye historia ya soka la Ufaransa tangu Kampuni ya Opta ilipoanza kurekodi data msimu wa 1950-51.

Mbappe ana mabao tisa na asisti 14 kwa jina lake kwenye Ligue 1 msimu huu kwa kikosi hicho cha kocha, Mauricio Pochettino, ambacho kinaongoza msimamo wa ligi hiyo.

Asisti ya Messi kwa bao hilo la Mbappe inamaanisha kwamba nyota huyo wa zamani wa Barcelona amehusika katika mabao kwenye mechi mfululizo kwa mara ya kwanza katika maisha yake hapo PSG.

Alifunga mara mbili dhidi ya Club Brugge kwenye Ligi ya Mabingwa katikati ya wiki na anakatoa pia asisti.

MECHI KALI
HOME
AWAY
BRENTFORD
3.95 | 3.56 | 1.90
MANCHESTER UTD
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE KASINO



# KIMMICH SASA AKUBALI KUCHANJA

**MUNICH,** Ujerumani

JOSHUA Kimmich ameelezea majuto yake kwa kukataa kupata chanjo ya virusi vya corona, lakini wamewajia juu wale wote waliomshutumu kwa kusita kwake.

Kiungo huyo wa Bayern Munich na Ujerumani sasa amethibitisha kwamba yupo tayari kupata chanjo baada ya miezi kadhaa ya kusita, na pia kupata uzoefu wa maambukizo ya virusi hivyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, alizua gumzo kubwa Oktoba wakati alipoelezea kwamba, hatakuwa tayari kuchoma sindano ya chanjo kwa kile alichokielezea kuwa haijafanyiwa utafiti wa kutosha kuhusu athari zake za muda mrefu.

"Kiukweli, ilikuwa ngumu kwa upande wangu kuamua kupata chanjo na hii ilikuwa ni kuhusu woga wangu binafsi, kitu ambacho sasa nimeamua baada ya kufikiria kwa muda mrefu," alisema Kimmich akinukuliwa na Televisheni ya Ujerumani ya ZDF.

"Pengine sasa natakiwa kupata chanjo baada ya kile nilichokipitia. Bila shaka nikiangalia nyuma, nilitakiwa kupata chanjo hii mapema zaidi, lakini wakati huo haikuwa rahisi kwa upande wangu."

Kimmich hajaichezea Bayern tangu



# Ancelotti: Naamini Real Madrid itabeba LaLiga

**MADRID,** Hispania

CARLO Ancelotti anaamini Real Madrid ni "wazi wana nafasi kubwa" kuwa mabingwa wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, baada ya kupata ushindi wa mabao 2-0 katika mchezo wa dabi ya jiji moja dhidi ya Atletico Madrid, Jumapili.

Vinara hao wa LaLiga, Madrid wamejikita kileleni wakiongoza kwa tofauti ya pointi 13 dhidi ya Atletico waliopo nafasi ya nne, kwa mabao kutoka kwa Karim Benzema na Marco Asensio na kufikisha mechi 11 bila kufungwa dhidi ya wapinzani wao hao.

Ulikuwa ni ushindi wa saba mfululizo kwa Madrid kwenye Ligi Kuu na kumewafanya kuongoza kwa tofauti ya pointi saba dhidi ya Sevilla waliopo nafasi ya pili, ingawa kikosi hicho cha kocha Unai Emery kina mchezo mmoja mkononi.

Alipoulizwa kuhusu matokeo ya tim
yake hiyo, Ancelotti aliwaambia waan
shi wa habari: "Nafikiri matokeo ya A
celotti; nina timu inanifanya nitulie k
sababu ya kile wanachokifanya dimba

"Wanamiliki mchezo vizuri sana
wanafanya vizuri mno kwenye ulinzi.
timu ambayo haina tena wachezaji
daraja la juu, lakini ni wanaojituma sa

"Kwa uwazi kabisa sisi tuna naf
kubwa ya (kushinda taji hili) kwa saba
tumefanya vizuri sana, bora kuliko w
gine, lakini mara zote huwa tunaanga
mchezo unaofuata.

"Na hiyo ndio njia pekee ya kukarib
ushindi na kushinda. Kwa vyovyote
ona kwamba nafasi yetu ni kubwa m
na tumeimarika tangu mwanzoni m
msimu huu."

LIVE IN PLAY

# BADRU APEWA MIKOBA YA LWANDAMINA AZAM

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Azam FC, umesitisha mkataba wa walimu wao wawili; Kocha Mkuu, George Lwandamina na msaidizi wake, Vivier Bahati kwa sababu ya mwenendo mbaya wa matokeo ya timu hiyo.

**Hatua hiyo ni baada ya Azam FC, msimu huu kuanza kwa kusuasua katika michezo yao ya msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara.**

Azam FC walimwongeza mkataba wa mwaka mmoja kocha Lwandamina baada ya kumalizika mechi dhidi ya Yanga, iliyopigwa Oktoba 30, mwaka huu.

Taarifa za uhakika zilizofikia gazeti hili kutoka ndani ya timu hiyo, kutokana na kutofanya vizuri katika ligi uongozi umechukuwa maamuzi ya kuwaondoa makocha hao huku kocha wa timu ya vijana, Mohammed Badru akipewa jukumu la kukaimu nafasi hiyo kwa muda hadi hapo uongozi utakapomtangaza kocha mpya atakayerithi mikoba ya Lwandamina.

"Mwenendo wa timu si mzuri, tumekutana na makocha hao na kukubaliana kusitisha mikataba yao. Kocha wetu wa Vijana, Badru atakuwa sehemu ya benchi hadi atakapotangazwa kocha mpya," alisema mtoa habari huyo.

Walipotafutwa viongozi wa Azam FC, akiwamo Mtendaji Mkuu, Abdulkarim Amin 'Popat' na Ofisa Habari, Zakaria Thabiti 'Zaka za Kazi' hawakupokea simu hadi gazeti linaenda mtamboni.

Azam FC iko nafasi ya saba ikiwa na pointi 11 baada ya kushuka dimbani mara nane ikishinda mitatu, sare mbili na kupoteza mechi tatu.



George Lwandamina. **PICHA: MAKTABA**

# *Kilimanjaro Premium Lager kuja na marathon kubwa zaidi mwakani*

**Na Mwandishi Wetu**

MDHAMINI Mkuu wa mbio maarufu za Kilimanjaro Marathon, Kilimanjaro Premium Lager, ameahidi mbio kubwa zaidi zenye matukio ya kusisimua wakati zikitimiza miaka 20 tangu kuanzishwa kwake.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Meneja wa Bia ya Kilimanjaro Premium Lager, Irene Mutiganzi, alisema wakati huu ikiwa imebaki miezi miwili na nusu kabla ya kufanyika kwa mbio hizo, wao kama wadhamini wakuu wanashirikiana kwa karibu na waandaaji kuhakikisha shughuli hiyo ya miaka 20 inafana sana.

"Mashindano yajayo ya Kilimanjaro Marathon yatakuwa ya hatua muhimu haswa ikitiliwa maanani kuwa chapa ya Kilimanjaro Premium Lager imekuwa mdhamini mkuu wa mbio hizo tangu kuanzishwa kwake miaka 20 iliyopita.

"Tunatarajia kuyafanya mashindano hayo ya maadhimisho ya miaka 20 kwa namna ya kipekee, kwani ni ya kihistoria kutokana na ukweli ni moja ya udhamini mrefu kupitia chapa ya Kilimanjaro Premium Lager na ambayo imeifanya chapa hiyo kukua mwaka hadi mwaka," alisema na kuongeza, kuwa wameguswa pia na umuhimu wa mashindano haya kukuza utamaduni wa Mtanzania pamoja na utalii kwa ujumla.

"Tumetenga zawadi za fedha zenye thamani ya jumla ya Sh. milioni 22, ambapo washindi wa kwanza katika mbio za Km. 42 kwa wanawake na wanaume watapata zawadi ya shilingi milioni nne kila mmoja," alisema na kuongeza kuwa katika mbio hizo za kilometa 42 kutakuwa na motisha ya ziada ya Sh. milioni 1.5 kwa kila Mtanzania atakayemaliza wa kwanza upande wa wanaume na wanawake," alisema.

Aidha, alitoa wito kwa washiriki kujiandikisha mapema kwa kuwa zoezi hilo limeanza tangu Oktoba 17, mwaka huu, kupitia anuani ya mtandao www.kilimanjaromarathon.com na kupitia Tigo Pesa kwa kupiga * 149 * 20 #.

"Nitoe wito kwa wanaotarajia kushiriki mbio hizi kuchangamkia fursa ya punguzo la asilimia 20 kwa wale watakaojiandikisha sasa hadi Januari 7, mwakani kwani baada ya hapo watakaojiandikisha watalipa malipo yaliyowekwa na waandaaji.

"Sisi kama TBL tutawakilishwa na baadhi ya wafanyakazi ambao watakimbia mbio tofauti tofauti na tayari wameshaanza mazoezi ili kujiandaa na mbio hizi kubwa Afrika Mashariki na Kati ambazo huleta pamoja washiriki zaidi ya 11,000 kutoka mataifa zaidi ya 55," alisema.

Wadhamini wa mbio hizo zitakazofanyika Februari 27, mwakani katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi ni Kilimanjaro Premium Lager- Km. 42, Tigo- Km. 21 (Half Marathon), Grand Malt- Kilometa tano, huku wadhamini wa meza za maji ni Absa, Unilever, TPC Sugar, Simba Cement, Kilimanjaro Water, na wasambazaji maalumu, GardaWorld Security, Keys Hotel, Kibo Palace Hotel na CMC Automobiles.


SPORTPESA APP

BET LEO UWE MILIONEA




MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 14 - DESEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:30 | 4033 | Singapore vs Timor-Leste | 1.01 | 13.55 | 43.55 |
| 15:45 | 5075 | Laci vs KF Tirana | 1.66 | 3.35 | 5.04 |
| 16:30 | 2107 | Amazulu vs Chippa Utd | 1.89 | 3.04 | 4.52 |
| 17:00 | 5143 | Venezia vs Ternana | 1.65 | 4.04 | 4.54 |
| 18:00 | 2559 | Tshakhuma vs Cape Town City | 2.98 | 3.03 | 2.41 |
| 18:15 | 2871 | Asteras Tripolis vs Panetolikos | 1.64 | 3.70 | 5.13 |
| 18:30 | 1986 | Clinceni vs Voluntari | 3.68 | 3.14 | 2.04 |
| 18:30 | 4360 | Mamelodi Sundowns vs Baroka FC | 1.26 | 5.13 | 10.84 |
| 19:00 | 3002 | Altinordu vs Kocaelispor | 3.42 | 3.51 | 1.91 |
| 20:00 | 3125 | Udinese vs Crotone | 1.32 | 5.31 | 7.86 |
| 20:00 | 4460 | PEC Zwolle vs Maastricht | 1.33 | 4.80 | 7.30 |
| 20:00 | 5613 | ADO Den Haag vs VV Gemert | 1.01 | 14.48 | 28.95 |
| 20:30 | 2060 | Moroka Swallows FC vs Orlando Pirates | 3.30 | 2.71 | 2.45 |
| 20:30 | 2785 | Stuttgart vs Bayern Munchen | 8.97 | 6.38 | 1.26 |
| 20:45 | 1075 | Radomiak Radom vs GKS Piast Gliwice | 1.95 | 3.27 | 3.56 |
| 20:45 | 3954 | Cercle Brugge vs RFC Seraing | 1.58 | 4.03 | 5.11 |
| 21:00 | 1199 | San Sebastian Reyes vs Fuenlabrada | 3.30 | 3.10 | 2.23 |
| 21:00 | 2114 | Viseu vs Benfica Lisbon B | 3.18 | 3.23 | 2.17 |
| 21:00 | 4160 | Halmstads BK vs Helsingborg | 1.69 | 3.48 | 4.54 |
| 21:00 | 5560 | FC Andorra vs Celta Vigo | 7.87 | 4.72 | 1.36 |
| 21:30 | 3109 | Universitatea Craiova vs UTA Arad | 1.89 | 3.24 | 4.12 |
| 21:30 | 5182 | SC Kriens vs FC Aarau | 3.53 | 3.67 | 1.84 |
| 22:00 | 1110 | Rayo Majadahonda vs Malaga | 3.45 | 3.11 | 2.16 |
| 22:00 | 1241 | Le Mans vs Cholet | 1.71 | 3.66 | 4.40 |
| 22:00 | 1827 | Zaragoza vs Burgos | 1.92 | 3.32 | 3.96 |
| 22:00 | 2265 | Huesca vs Girona | 2.25 | 3.20 | 3.15 |
| 22:00 | 4339 | Emmen vs Excelsior Maassluis | 1.10 | 8.08 | 15.40 |
| 22:30 | 3627 | VfL Wolfsburg vs FC Koln | 2.05 | 3.49 | 3.44 |
| 22:30 | 3854 | Mainz vs Hertha BSC | 1.78 | 3.63 | 4.38 |
| 22:30 | 4463 | Brentford vs Manchester Utd | 3.95 | 3.56 | 1.90 |
| 22:30 | 5159 | Arminia Bielefeld vs VfL Bochum | 2.41 | 3.29 | 2.89 |
| 22:45 | 1795 | Leiston vs Stratford Town | 2.30 | 3.86 | 2.46 |
| 22:45 | 2524 | Hayes Yeading United vs Truro City | 1.42 | 4.53 | 5.78 |
| 22:45 | 2843 | Hibernian vs Dundee FC | 1.65 | 3.64 | 5.12 |
| 22:45 | 3892 | Barwell vs Stourbridge | 2.28 | 3.94 | 2.45 |
| 22:45 | 3908 | Norwich City vs Aston Villa | 3.20 | 3.30 | 2.25 |
| 22:45 | 4068 | Hendon vs Gosport Borough | 2.39 | 3.80 | 2.39 |
| 22:45 | 4314 | Margate vs Worthing | 3.95 | 3.71 | 1.73 |
| 22:45 | 5065 | Eastleigh vs Solihull Moors | 2.53 | 3.40 | 2.53 |
| 22:45 | 5725 | Flint Town United vs Caernarfon Town | 1.72 | 3.85 | 3.85 |
| 22:45 | 5876 | Halifax vs Kings Lynn | 1.51 | 4.29 | 5.26 |
| 23:00 | 1363 | Telstar vs SV Spakenburg | 1.24 | 5.79 | 8.49 |
| 23:00 | 1399 | Genoa vs Salernitana | 2.16 | 3.39 | 3.15 |
| 23:00 | 2305 | Anderlecht vs St Truiden | 1.33 | 5.14 | 7.92 |
| 23:00 | 2989 | Oostende vs Kortrijk | 2.56 | 3.40 | 2.56 |
| 23:00 | 4340 | Alcoyano vs Levante | 6.33 | 4.35 | 1.45 |
| 23:00 | 4748 | CD Cristo Atletico vs Espanyol | 27.72 | 8.91 | 1.08 |
| 23:00 | 4750 | NAC Breda vs Utrecht | 3.61 | 3.61 | 1.83 |
| 23:00 | 5745 | Manchester City vs Leeds | 1.17 | 7.07 | 15.54 |
| 23:00 | 5984 | CD Linares vs Alaves | 6.33 | 4.35 | 1.45 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.